

# USAFIRI ARDHINI

Toleo la 01
Januari - Juni, 2023
ISSN 2961- 6255

## UFAHAMU MFUMO WA VTS NA JINSI UNAVYOFANYA KAZI

"Baada ya kuona gari linaenda mwendo kasi zaidi ya unaotakiwa, tunaangalia ni gari gani na kisha tunampigia mmiliki ili kumuarifu kuhusu dereva wa chombo chake anavyoendesha kwa mwendokasi"...... Uk. 3

## MABASI 22 YAFUNGIWA KWA KUCHEZEA VTS

"Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tunadhibiti kila upande ili kuhakikisha kwamba madereva wana sehemu yao ya kuwajibika lakini pia wamiliki wa magari wana sehemu yao ya kuwajibika,"..... Uk. 9

## LATRA YAONGEZA SIKU 90 KWA MADEREVA KUJISAJILI

"Kwa usajili huu madereva wanakuwa wamekidhi kupata uhalali wa kupata ajira katika nchi yeyote ambayo nchi yetu ni mwananchama mwenza, pia tunaweza kutambua kwa muda Fulani ni dereva gani…" UK 27

# MHE. MAJALIWA : LATRA NA TAMISEMI WAPATIENI ELIMU MADEREVA

# TAHARIRI



Karibu katika toleo la kwanza na rasmi la jarida la USAFIRI ARDHINI kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ambalo linaandaliwa na kusambazwa mara nne kwa mwaka.

Jarida hili limekusanya taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ambazo zimefanyika ndani ya nusu ya kwanza ya Mwaka 2023, yaani kuanzia mwezi Januari mpaka Juni mwaka 2023. Lengo la jarida hili ni kukuhabarisha mdau wetu kuhusiana na mambo ya msingi yanayotekelezwa na Mamlaka ikiwa ni sehemu ya utoaji elimu kuhusu shughuli za Mamlaka na masuala mbalimbali yanayogusa sekta ya Usafiri Ardhini.

Katika kipindi cha mwanzo wa mwaka LATRA imetangaza nauli mpya za Mabasi Yaendayo Haraka na Teksi Mtandao kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413. Mamlaka imefanikisha kwa kiwango kikubwa kutangaza na kusimamia nauli hizo, hii ni kwa kuhakikisha tiketi zinatolewa kwa abiria ni zile za kielektroni au kadi ambazo zinakubalika na watoa huduma pamoja na kutoa elimu kwa abiria kuwa wazingatie wanaposafiri wapewe tiketi za kielektroni zenye nauli halali kama ilivyotangazwa na Mamlaka.

Aidha tumeendelea kutoa elimu na wito kwa madereva wanaoendesha mabasi na magari ya mizigo kuondoa hofu na kujitokeza kwa wingi ili kusajiliwa na kufanyiwa ithibati. Moja ya faida ya kuwasajili na kuwafanyia ithibati madereva ni dereva kutambulika rasmi na tutakuwa na taarifa kamili ya dereva yupi anaendesha chombo kipi kwa wakati husika. LATRA imekubaliana na baadhi ya wadau wengine wakiwemo Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) kuwa madereva wataruhusiwa kuendesha mabasi wakiwa wamesajiliwa huku wakifuatiliwa mienendo yao ya uendeshaji.

Katika kuendelea kusimamia usalama wa watumiaji wa huduma za usafiri ardhini, Mamlaka imeshiriki katika maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yaliyofunguliwa rasmi na Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho hayo yaliyofanyika Jijini Mwanza Machi 14 hadi 18, 2023 lengo ikiwa ni LATRA kutoa elimu ya namna inavyoshiriki kudhibiti ajali za barabarani.

Vilevile, katika kuboresha usafiri wa ardhini Mamlaka imekabidhi vifaa vya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ikiwemo runinga mbili, kompyuta mbili pamoja na kompyuta mpakato mbili kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani. Makabidhiano hayo yamefanyika Machi 31, 2023 kwa lengo la kudhibiti hali ya usalama kwa vyombo vya moto viwapo safarini na kupunguza ajali nchini.

Pamoja na hayo Mamlaka imezindua Jopo la kupitia maamuzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini linaloundwa na wajumbe wa nne (4) ambao ni Bw. Mohamed Mpinga, Mha. John Ngaraguza. Wakili Theresia Clemence pamoja na Wakili Asma Mohamed ambapo imezinduliwa rasmi June 2, 2023.

Hayo ni baadhi tu kati ya mengi utakayosoma kwa kina katika Jarida hili la USAFIRI ARDHINI. nami nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kufahamu vizuri maendeleo ya sekta ya Usafiri Ardhini na Udhibiti wa huduma za Usafiri Ardhini nchini.

Nakutakia usomaji mwema



**CPA Habibu J. S. Suluo**

# MHE. MAJALIWA: LATRA NA TAMISEMI WAPATIENI ELIMU MADEREVA WA PIKIPIKI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuratibu na kuwapa elimu madereva wa pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda).

Mhe. Majaliwa ameyasema hayo wakati akifungua rasmi maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani mwaka 2023 yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, ambayo kitaifa yameadhimishwa Jijini Mwanza kuanzia Jumanne Machi 14, 2023 hadi Jumamosi Machi 18, 2023.

"Niwatake LATRA, mshirikiane na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuwafikia wasafirishaji wadogo wadogo maarufu kama bodaboda, kaeni nao pamoja wapatiwe elimu juu ya namna bora ya kuendesha vyombo vyao kwa usalama, lakini pia waratibiwe ili wajue namna bora ya kuendesha biashara yao," amesema Mhe. Majaliwa.

Aidha Mhe. Majaliwa amewataka Wananchi wa Mwanza na Tanzania kwa jumla kuwa mstari wa mbele katika kukemea vitendo ambavyo vinaweza kusababisha ajali na kupelekea athari kubwa kwa Watanzania.

"Nimetazama igizo moja mtandaoni, abiria amemnyang'anya siti dereva kwa sababu dereva alikuwa anaongea na simu huku anaendesha, mara anashuka bila sababu ya msingi, akasema gari halitoki mpaka aje dereva mwingine, na nyie muwe hivyo, mkiona uendeshaji hatarishi msikae kimya, toeni taarifa kwa Mamlaka husika, hapo kila mtu atakuwa ametimiza wajibu wake na Tanzania bila ajali itawezekana," ameongeza Mhe. Majaliwa.



*Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza na wadau mbalimbali waliohudhuria ufunguzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2023 jijini Mwanza*

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Jumanne Sagini (Mb) amewataka wamiliki wa vyombo vya moto kufuata maelekezo yaliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Mha. Hamadi Masauni (Mb) na kufunga vidhibiti mwendo katika Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

"Kuhusu swala la kuchagua kimoja kati ya kudhibiti mwendo au VTS inayobeba dhana zote mbili, Waziri mwenye dhamana Mhe. Masauni ameshatoa maelekezo kuwa kwa kuwa vifaa vya VTS vinaweza kufungwa vidhibiti mwendo basi wamiliki wa magari ya kusafirisha abiria wafunge vidhibiti mwendo kwenye mfumo huo," amesema Mhe. Sagini.

Akiongelea jitihada zilizofanywa na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani katika kudhibiti ajali kutoka kwa madereva wa Serikali, Mhe. Sagini amesema Baraza kwa kushirikiana na LATRA, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) waliendesha mafunzo ya usalama barabarani kwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuhakikisha madereva wao wanachukua tahadhari.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Ajali kwa mwaka 2022, makosa ya kibinadamu bado yanachangia kwa kiasi kikubwa ajali zinazotokea nchini, hivyo basi ni vyema kila mmoja wetu akatimiza wajibu wake kikamilifu ili kuhakikisha tunapunguza hatari ya ajali tuwapo safarini.



*Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb), Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) akizungumza na Watumishi wa Sekta ya Uchukuzi katika Bonanza la Uchukuzi*

# MHE. MWAKIBETE: WAKUU WA TAASISI MUWARUHUSU WATUMISHI KUSHIRIKI MICHEZO

Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb) amewataka Wakuu wa Taasisi walio chini ya Wizara yake kuwaruhusu watumishi wanamichezo kushiriki kwenye mabonanza mbalimbali ili kuimarisha afya zao.

Mhe. Mwakibete amesema hayo Januari 21, 2023 alipokuwa akifungua bonanza la Sekta ya Uchukuzi lililodhaminiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na kufanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Mhe. Mwakibete amesema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa watumishi kufanya mazoezi ili kuboresha afya zao. Hivyo amewapongeza watumishi wa Sekta ya Uchukuzi kwa kuandaa na kushiriki bonanza hilo ambalo linaonesha dhahiri namna wanavyotekeleza agizo la Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza mara kwa mara kuwa wananchi wafanye mazoezi kwa mustakabali mzuri wa afya zao na kwa hili mlilolifanya hapa leo kiukweli mmeonesha kwa vitendo kuwa mnatekeleza maono ya Rais wetu kwa vitendo", amesisitiza Mhe. Mwakibete.

Vilevile Mhe. Mwakibete amewataka Wakuu wa Taasisi kuhakikisha wanatenga bajeti ya kutosha ili kuwawezesha watumishi wanamichezo kushiriki kikamilifu kwenye michezo na amesisitiza Wizara itahakikisha inasimamia utekelezaji wa jambo hilo.

"Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kwenye matibabu ya wananchi wake kwa sababu ya kutofanya mazoezi, hivyo ninaendelea kuwasihi kufanya mazoezi kila mara ili kuepukana na magonjwa yanayosababishwa na tabiabwete," ameeleza Mhe. Mwakibete.

Wakati huohuo Mhe. Mwakibete amezindua Jarida la Klabu ya Sekta ya Uchukuzi na amewapongeza viongozi wa Klabu hiyo kwa kubuni na kuandaa jarida hilo litakalotoa taarifa mbalimbali za michezo ya Sekta ya Uchukuzi.

Naye Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA. Habibu Suluo amemshukuru Mhe. Mwakibete kwa kujumuika pamoja kwenye bonanza hilo na amesema michezo ni afya, inaleta umoja na inaongeza ufanisi katika maeneo ya kazi.

"Ushiriki wako hapa leo umetupa nguvu kubwa ya kuendeleza michezo hii na tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu uliopo miongoni mwetu kupitia michezo," ameeleza CPA Suluo.

Naye Katibu wa Klabu ya Uchukuzi Bw. Mbura Tenga amesema hilo ni bonanza la tano kuandaliwa na Sekta ya Uchukuzi na ameishukuru LATRA kwa kudhamini kwa asilimia 100.

# WASAFIRISHAJI WATAKIWA KUUNGANISHA MFUMO WA TIKETI MTANDAO NA MFUMO WA TRA

Wadau wa usafirishaji wametakiwa kuunganisha Mfumo wa Tiketi Mtandao na Mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwezesha taarifa za ukataji wa tiketi kufika moja kwa moja kwenye Mamlaka hiyo.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw. Johansen Kahatano kwenye kikao cha pamoja na wadau wa usafirishaji, kilichofanyika katika ofisi za LATRA Dar es Salaam Januari 25, 2023 ambacho kilihudhuriwa na wadau kutoka Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kituo cha kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC).

Bw. Kahatano amesema, “Wapo watoa huduma wachache waliounganisha mfumo wao na TRA lakini wengine bado hawajafanya hivyo, na tumepeana muda mpaka kufikia Januari 31, 2023 wadau wote wawe wameshaunganisha mifumo yao kwenye mfumo mama wa TRA ili taarifa zote za tiketi zinazokatwa zionekane TRA kwa lengo la kufuatilia mapato yanayotokana na huduma ya usafirishaji.”

Kwa upande wake Katibu Mkuu Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) Bw. Joseph Priscus, amesema wao kama wasafirishaji wametoa maoni yao kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwamba baadhi ya Sheria zake zinazosimamia upande wa mabasi ziendane na mazingira ya usafirishaji lakini pia Sheria ziweze kutenganisha makosa kati ya mmiliki wa chombo cha usafiri, dereva na kondakta.

“Tunaomba TRA watengeneze Sheria ambayo kila mtu awajibishwe kwa kosa lake kama vile kosa la dereva awajibike dereva, kosa la kondakta awajibike kondakta na kosa la mmiliki wa gari awajibike mmiliki. Lakini tunashukuru tumesikilizwa kuna mambo yanaenda kufanyiwa kazi na TRA,” ameeleza Bw. Priscus.

Naye Bw. Gerald Katawanya, Meneja Mradi kutoka Kituo cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC) ameshukuru kwa kushirikishwa kwenye kikao hicho na amesisitiza suala la utoaji wa elimu kuhusu Tiketi Mtandao kwa watumiaji lakini pia kwa baadhi ya wasafirishaji ambao bado hawajaanza kutoa huduma kupitia Tiketi Mtandao ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa katika mfumo huo.

“Mfumo wa Tiketi Mtandao una umuhimu na faida kubwa ikiwemo kuokoa muda ambao abiria anatumia wakati wa kwenda kukata tiketi katika ofisi za mabasi, kuepuka changamoto za wapiga debe lakini pia husaidia abiria kupata stahiki zake endapo itatokea ajali au madhara yoyote kwa kupewa fidia na bima,” amefafanua Bw. Katawanya.



***Baadhi ya wadau mbalimbali waliohudhuria kikao cha pamoja kilichoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika ofisi za LATRA Dar es Salaam.***

# MHE. SENYAMULE: LATRA EPUKENI RUSHWA, CHUKUENI HATUA DHIDI YA WAVUNJA SHERIA



*Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma akizungumza na wafanyakazi wa LATRA katika hafla ya uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi*

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, amewaagiza wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuchapa kazi kwa kuzingatia uweledi, kuepuka vitendo vya rushwa na kuchukua hatua dhidi ya madereva na wasafirishaji wanaokiuka Sheria za matumizi sahihi ya miundombinu ya usafirishaji.

Mhe. Senyamule ameyasema hayo tarehe 26 Januari, 2023 katika hafla ya uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi wa LATRA iliyofanyika Makao Makuu ya LATRA Jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo Mhe. Senyamule amesisitiza kuwa, Serikali kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi katika kuendeleza miundombinu ya barabara na reli nchini, hata hivyo kuna baadhi ya madereva na wasafirishaji wanashindwa kutimiza wajibu wao na kusababisha maafa na taharuki kwa watumiaji wengine wa miundombinu hiyo.

Aidha, amesema kuwa mazingira ya wafanyakazi wa LATRA yanavishawishi vingi kutokana na mgongano wa maslahi ya watoa huduma mbalimbali hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa uweledi na uadilifu ili kuboresha huduma inayotolewa kwa wananchi na kuepusha migogoro.

“Sisi Dodoma tumebahatika kupata miundombinu mizuri ya usafiri wa barabara na reli, LATRA muendelee kutoa elimu ya matumizi sahihi ya miundombinu kwa umakini na kwa kufuata taratibu sahihi ili kukamilisha azma ya Serikali ya kuwezesha maisha bora kwa Watanzania”, amesema.

Pia ametoa rai kwa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji (COTWU) kuleta mshikamano wa wafanyakazi na kushirikiana na Menejimenti ili kuongeza tija na kuepusha migogoro mahala pa kazi.

> **“Baraza la Wafanyakazi ndio jukwaa la Kisheria la Majadiliano ya pamoja kati ya viongozi wa taasisi na wafanyakazi. Uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

“Baraza la Wafanyakazi ndio jukwaa la Kisheria la Majadiliano ya pamoja kati ya viongozi wa taasisi na wafanyakazi. Uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwaka 1970 na ni utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 kifungu cha 73 kinachoelekeza juu ya kutekeleza sera ya kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi na ni nguzo ya utawala bora,” amesema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria, Baraza hilo linapaswa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka, mara ya kwanza linapopitisha mpango na bajeti ya taasisi na mara ya pili linapofanya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa nusu mwaka. Hivyo, amewapongeza washiriki wote kwa kukamilisha taratibu za kisheria kwa kuunda Baraza la Wafanyakazi lililosajiliwa na Kamishna wa Kazi kwa mujibu wa Sheria.

Wakati huo huo, Mhe. Senyamule ameipongeza LATRA kwa kuhamia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma na kuwakaribisha katika mkoa huo ulio na fursa lukuki za maendeleo.

“Natumia fursa hii kuwakaribisheni sana hapa Dodoma, Makao Makuu ya

Inaendelea uk.7 >>

## MHE. SENYAMULE: LATRA EPUKENI RUSHWA, CHUKUENI HATUA DHIDI YA WAVUNJA SHERIA

<< Inatoka uk.6

Nchi yetu. Nafahamu kwamba LATRA ni miongoni mwa Taasisi zilizotekeleza Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma, na ninayo taarifa Ofisi yenu ya Makao Makuu ilihamia rasmi Dodoma tarehe 26 Septemba, 2022 ambapo leo tarehe 26 Januari, 2023 mnatimiza miezi minne kamili. Karibu sana Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makao Makuu," amesisitiza.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo, amempongeza Mkuu wa Mkoa huo kwa kusimamia kwa ufanisi maendeleo ya mkoa wa Dodoma na kuwa LATRA itaendelea kushirikiana na Uongozi wa mkoa kuongeza ufanisi katika huduma za usafiri ardhini.

"Mkoa wa Dodoma unapendeza, ratiba zetu na leseni tunazotoa kwa mabasi zinawezesha usafiri kutoka Dodoma kwenda mikoa yote Tanzania Bara na kufika siku hiyo hiyo," ameeleza.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi COTWU, tawi la LATRA Bw. Patel Ngereza amesema kuwa, Wafanyakazi wa LATRA wanampongeza Mkurugenzi Mkuu, CPA Habibu Suluo kwa kufanya maboresho makubwa katika utendaji wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na kusikiliza na kutatua kero za wafanyakazi, kutekeleza kwa vitendo ushirikishwaji wa wafanyakazi katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka na kushirikisha kwa karibu wadau mbalimbali wakiwemo wasafirishaji, Jeshi la Polisi na taasisi za Serikali tangu alipoteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Julai, 2022.

"Kutokana na juhudi za uongozi wa LATRA, sisi viongozi tunaendelea kuhamasisha Wafanyakazi wa LATRA kuchapa kazi kwa bidii, ubunifu na kuwajali wateja wetu huku tukiomba Menejimenti kuendelea kutimiza mahitaji ya wafanyakazi katika mahala pa kazi," amesema.




*Mfanyakazi wa LATRA akiwa katika shughuli za kila siku za ukaguzi na utoaji elimu kwa wasafirishaji eneo la Mbagala, Dar es Salaam.*

# HABARI PICHA



*Mha. Hanya Mbawala, Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli akifanya ukaguzi katika mabehewa mapya ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) yanayotengenezwa nchini Korea.*



*Mha. Hanya Mbawala, Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli pamoja na Mha. Elisha Mhoka, Mkaguzi wa Reli Mwandamizi wakifanya ukaguzi katika mabehewa mapya ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) kabla ya kuanza kutumika.*



*Wadau mbalimbali waliohudhuria mkutano wa wasafirishaji watalii ulioandaliwa na LATRA jijini Arusha.*



*Wadau mbalimbali waliohudhuria mkutano wa wasafirishaji watalii ulioandaliwa na LATRA jijini Arusha katika picha ya pamoja.*



*Bw. Salum Pazzy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano LATRA akitoa elimu kwa wadau wa usafiri ardhini mkoani Manyara.*

# PROF. AME AHIMIZA MAADILI, KUCHAPA KAZI NA MATUMIZI YA TEHAMA



*Prof. Ahmed Mohammed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA akikagua mitambo ya Kanzi Data ya VTS.*

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA Prof. Ahmed Mohammed Ame aliyeteuliwa tarehe 15 Januari, 2023 ameongoza kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika Februari 7, 2023 LATRA Makao Makuu jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa kikao hicho Prof. Ame alisema kuwa anamshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumuamini katika nafasi hiyo.

Aidha, amewakumbusha wajumbe wa menejimenti na wafanyakazi wa LATRA kuchapa kazi kwa kuzingatia maadili na ubunifu ikiwemo matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza tija katika kuwahudumia Watanzania.

Pia amewasihi wajumbe wa Menejimenti kuimarisha ushirikishwaji wa wafanyakazi katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo baraza la wafanyakazi na viongozi kujishusha ili wafanyakazi watoe mawazo yao kwa uhuru.

"Ratiba ya vikao vya baraza la wafanyakazi ijulikane mapema na iheshimiwe, haipendezi kubadilisha tarehe ya mkutano wa baraza kwa kuwa wafanyakazi huwa wanajipanga kuwasilisha hoja mbalimbali na ukibadilisha ratiba huwa wanajisikia kutothaminiwa," amefafanua.

Aidha, amesisitiza Mamlaka kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuajiri wafanyakazi kwa kutoa kipaumbele kwa wanawake wenye sifa zinazohitajika ili kuboresha uwiano wa kijinsia.

Kuhusu ushiriki wa wafanyakazi katika michezo, Mwenyekiti huyo wa Bodi amesisitiza wafanyakazi washiriki katika michezo na kuongeza kuwa yeye ni mpenzi wa michezo na akipata wasaa atashiriki katika michezo itakayoandaliwa. Pia, amesisitiza kufanya kazi kwa ukaribu na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa watoa huduma zinazodhibitiwa.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti huyo wa Bodi ametoa shukrani kwa wajumbe wa Bodi anayoiongoza, Menejimenti na Wafanyakazi wa LATRA na wadau wengine kwa salamu za pongezi na mapokezi mazuri aliyoyapata.

Aidha, Prof. Ame ameahidi kushirikiana na wajumbe wa Bodi hiyo na Menejimenti ili kuhakikisha kuwa malengo ya Mamlaka hiyo yanatekelezwa, "Tutafanya kazi kwa kushirikiana, panapohitaji kukumbushana tukumbushane na panapohitaji kukosoana tutakosoana," ameeleza.

Akizungumza kwa niaba ya Mhandisi Dkt. John S. Ndunguru, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA Wakili Tumaini Silaa alimkaribisha Prof. Ame na kumuahidi ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, alimkabidhi, Sheria ya LATRA Sura ya 413 na Kanuni zake, Sheria ya Leseni za Usafirishaji na Kanuni zake na Sheria ya Reli ikiwa ni sehemu ya vitendea kazi vitakavyotumika kutekeleza majukumu ya bodi hiyo.

# KASAGARA: WASAFIRISHAJI JIUNGENI KWENYE MFUMO WA TIKETI MTANDAO




*Bw. Emil Kasagara, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Mwanza akizungumza na wanachama wa TABOA waliohudhuria semina iliyoandaliwa na LATRA pamoja TRA mkoani Mwanza.*

Katibu Tawala Msaidizi (Seksheni ya Uchumi na Uzalishaji) Mkoani Mwanza Bw. Emil Kasagara amewataka wasafirishaji wa mabasi ya masafa marefu kujiunga na kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao na kuunganisha mifumo yao kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mashine za Risiti za Kielektroni (EFDMS) ili mifumo hiyo iweze kubadilishana taarifa.

Kasagara amesema hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Mwanza Mhe. Adam Malima kwenye semina kwa wanachama wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) iliyoandaliwa kwa ushirikiano wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iliyofanyika katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa Mwanza Februari 8, 2023.

Bw. Kasagara amesema kuwa, Mfumo wa Tiketi Mtandao unaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za uendeshaji wa Sekta ya usafirishaji nchini pamoja na kufanya maamuzi mbalimbali kwa usahihi na pia unasaidia kupunguza upotevu wa mapato kwa wamiliki kwa kuwa wanapata fedha zao pindi abiria anapokata tiketi yake.

"Mfumo huu ni mahususi kwa ajili ya usafiri wa abiria, unaruhusu mtu yeyote kukata tiketi bila ya kwenda stendi au kwenye ofisi ya basi husika, hii ni faida kwa wasafiri maana inaokoa muda na inawasaidia kupunguza adha wakati wa ukataji wa tiketI," ameeleza.

Aidha, amesema kuwa Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha utendaji wake kwa njia ya mifumo ambayo imeongeza tija na maendeleo ya nchi kwa jumla.

Naye Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao LATRA CPA Tadei Mwita amewasihi wasafirishaji kuzingatia Kanuni za Leseni za Usafirishaji - Mabasi ya Abiria za mwaka 2020 kwa kuwa ndizo zinazowaongoza katika utoaji wa huduma za usafirishaji nchini.

"Kanuni ya 22(j) inamtaka mwenye leseni ya kusafirisha abiria kutoa tiketi kwa kutumia mfumo wa tiketi wa Kielektroni ulioidhinishwa na LATRA na Kanuni ya 23(b) na 24(d) inamtaka mwenye leseni ya kusafirisha abiria ahakikishe tiketi ya kielektroni inatolewa kwa kila abiria," ameeleza CPA Mwita.

Ameongeza kuwa, Kanuni ya 30 inamtaka mtoa huduma ya usafiri wa abiria kutotoza nauli inayozidi kiwango kilichoidhinishwa kwa daraja husika la gari na Kanuni ya 32(1)(b) Mtoa huduma ya usafiri wa abiria ahakikishe wafanyakazi wa ndani ya gari wanapewa vifaa vya kuwawezesha kutoa tiketi za kielektroni.

Akizungumzia taarifa muhimu zinazotakiwa kuwekwa kwenye tiketi ya kielektroni, CPA Mwita amesema Kanuni ya 32(2)(a) inaelekeza tiketi iwe na Jina la abiria na namba ya siti, Muda wa abiria kufika na muda wa kuanza safari na Kituo cha kuanzia safari, njia itakayotumika na kituo cha mwisho cha safari.

Vilevile Kanuni ya 32(2) (a) Tiketi iwe na Nauli ya safari, Anwani na namba za simu za mtoa huduma, Namba ya gari, Tarehe ya tiketi kutolewa na tarehe ya safari pamoja na Namba ya tiketi (Serial number).

Kwa upande wake Mwakilishi wa Meneja TRA Mkoa wa Mwanza Bi. Millicent Igogo amesema TRA na LATRA wataendelea kushirikiana ili kuhakikisha kuwa wasafirishaji wanapata elimu na wanatumia Mfumo wa Tiketi Mtandao kwa kuwa umekuwa na tija kwa Serikali, Wamiliki na Wananchi kwa jumla.




*CPA Tadei Mwita, Meneja Mradi Tiketi Mtandao akizungumza na wamiliki wa mabasi katika semina iliyofanyika jijini Arusha.*

# WASAFIRISHAJI WAASWA KUZINGATIA KANUNI ZA LESENI ZA USAFIRISHAJI MAGARI YA ABIRIA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa wito kwa wasafirishaji kuzingatia Kanuni za Leseni za Usafirishaji Magari ya Abiria za mwaka 2020 ikiwemo ya kuwapatia abiria tiketi za kielektroni.

Hayo yameelezwa na Meneja Mradi Tiketi Mtandao CPA Tadei Mwita kwenye semina na wamiliki wa mabasi iliyofanyika Februari 12, 2023 jijini Arusha

CPA Mwita amesema Kanuni ya 22(j) inamtaka mwenye leseni ya kusafirisha abiria kutoa tiketi kwa kutumia mfumo wa tiketi wa Kielektroni ulioidhinishwa na LATRA na Kanuni ya 23(b) na 24(d) inamtaka mwenye leseni ya kusafirisha abiria ahakikishe tiketi ya kielektroni inatolewa kwa kila abiria.

"Kwa mujibu wa hizi kanuni, msafirishaji atapaswa kuhakikisha muda wote anapofanya kazi ya kusafirisha abiria anatoa tiketi kwa kutumia mfumo huu na kwa kila abiria anayepanda kwenye basi apewe tiketi ya kieletroni," amefafanua CPA Mwita

Vilevile amewaasa abiria kukata tiketi kwa kupitia simu janja ili kuepuka usumbufu wa wapiga debe kwenye vituo vya mabasi, "Tuwaombe abiria wasihangaike kwenda kwenye vituo vya mabasi wakate tiketi popote walipo bila kulazimika kwenda kwenye kituo cha mabasi lakini kwa upande wa usafirishaji wahakikishe mabasi yanapatikana kwenye mifumo ili abiria aweze kujihudumia pale alipo."

Aidha, CPA Mwita amewasihi wamiliki hao kuendelea kusoma na kuzifuata Kanuni za Usafirishaji Magari ya Abiria za mwaka 2020 zinazopatikana kwenye tovuti ya Mamlaka kupitia anwani www.latra.go.tz

Naye Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Bw. Salum Pazzy, amesema LATRA imekutana na wamiliki hao ili kuwapatia elimu ya matumizi ya tiketi mtandao na kusikiliza changamoto zao hasa mkanganyiko wa matumizi wanayofanya na kushindwa kutambuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakati wa kufanya makadirio ya kodi.

"Wameeleza changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ya upotevu wa mapato ambapo kwa pamoja tumeona suluhisho mojawapo ni kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao," amesema Bw. Pazzy

Kwa upande wa Meneja wa EFD Bw. Mabula Sambayuka, amesema ni muhimu wasafirishaji kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao ili wanapotoa tiketi ziwe na vigezo vyote kwa kuondoa changamoto wanazokutana nazo hasa pale wanapotumia tiketi zisizo za kielektroni na kuonekana wanakwepa kodi.

Naye Bw. Haruna Kakiva alishiriki semina hiyo amesema ameridhishwa na ushirikishwaji kwa kuwa unaimarisha uhusiano kati yao wamiliki wa mabasi na Mamlaka husika ambazo ni LATRA na TRA.

# WASAFIRISHAJI WATAKIWA KUFUATA SHERIA ZA USALAMA BARABARANI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani imetoa elimu kuhusu namna bora ya kudhibiti ajali za bararani kwa madereva wa abiria na mizigo ili kuweza kupunguza vifo pamoja na athari zitokanazo na ajali za barabarani.

Akizungumza hivi karibuni, Afisa Mfawidhi LATRA mkoa wa Manyara Bw. Joseph Michael amasema katika kupunguza ajali hapa nchini, Serikali kupitia LATRA inafanya usajili na uthibitishaji wa madereva kwa kuwapima kupitia mtihani lengo ni kuwa na madereva walioiva na wanaofahamu masuala ya udereva ikiwemo la Sheria na alama za barabarani.

"Ni dhahiri kuwa madereva wanaothibitishwa na Mamlaka wanakuwa ni wenye ujuzi na uweledi hivyo tunaamini kupitia uthibitishaji unaofanywa na LATRA itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza na hatimaye kumaliza tatizo hili la ajali ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watanzania wengi," ameeleza Bw. Michael.

Aidha Bw. Michael amewakumbusha wasafirishaji suala la ukataji wa leseni ambazo zitawaruhusu kufanya biashara za usafirishaji na pia amewasisitiza wasafirishaji kuzingatia masharti ya leseni hizo.

Naye Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Babati, ASP. Joseph Makumu amewasihi madereva kutii Sheria za Usalama Barabarani zilizowekwa ili kuepukana na ajali, "Tunawataka madereva watii Sheria, na barabara zetu zinaongea kwa maana zina alama na michoro hivyo zinaelekeza wapi unatakiwa kulipita gari, wapi unatakiwa usimame na wapi unatakiwa uchukue tahadhari".

Naye Hussein Shabani mmoja kati ya madereva kutoka Manyara amesema "Tunawashukuru sana LATRA kwa ujio wao wa kutuelimisha, na pia nawashauri madereva wenzangu tuzingatie Sheria za Usalama barabarani kwa sababu sisi tunabeba dhamana ya maisha ya abiria tunaowapakia kwenye vyombo tunavyoviendesha."

> **"Ni dhahiri kuwa madereva wanaothibitishwa na Mamlaka wanakuwa ni wenye ujuzi na uweledi hivyo tunaamini kupitia uthibitishaji unaofanywa na LATRA itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza na hatimaye kumaliza tatizo hili la ajali**




***Bw. Joseph Michael (wa kwanza kulia), Afisa Mfawidhi LATRA mkoa wa Manyara akitoa elimu kwa baadhi ya wasafirishaji mkoani Manyara.***



*CPA Tadei Mwita, Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao kutoka LATRA akizungumza na wadau wa usafiri nchini kwenye semina ya utekelezaji wa Mfumo wa Tiketi Mtandao mkoani Tanga.*

> **"Kuna tatizo kubwa la ushindani hasi kwa wasafirishaji, wanatoa mabasi mengi kwa wakati mmoja na baadhi ya mabasi yanaenda yakiwa na upungufu wa abiria hivyo inawasababishia hasara kwao**



# WASAFIRISHAJI WAASWA KUFANYA KAZI KWA USHIRIKA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri (LATRA) imewaasa wasafirishaji kuungana na kuwa na ushirika wa pamoja ili kuondoa ushindani usio na tija na kuweza kuongeza kipato chao.

Hayo yameelezwa na Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao kutoka LATRA CPA Tadei Mwita kwenye semina ya utekelezaji wa Mfumo wa Tiketi Mtandao iliyoandaliwa kwa ushirikiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kutolewa kwa wamiliki wa mabasi mkoani Tanga Februari 14, 2023.

CPA Mwita amesema, "Kuna tatizo kubwa la ushindani hasi kwa wasafirishaji, wanatoa mabasi mengi kwa wakati mmoja na baadhi ya mabasi yanaenda yakiwa na upungufu wa abiria hivyo inawasababishia hasara kwao, kwa hiyo Mamlaka imekuja na mpango wa wasafirishaji watengeneze ushirika kama kampuni na Mamlaka itatoa leseni kwa kampuni au ushirika na hii italeta ufanisi kwa Mamlaka na tija kwa wasafirishaji."

Naye Bw. Mabula Sambayoka, Meneja wa EFD kutoka TRA amesema wamewaelimisha wasafirishaji kuhusu matumizi ya Mfumo wa Tiketi Mtandao na jinsi ya kuunganisha mfumo huo pamoja na mfumo wa ulipaji kodi ya mapato ili waweze kutimiza takwa la kisheria la ulipaji wa kodi ya mapato Tanzania.

Kwa upande wake Bw. Abdi Awadhi ambaye ni mwenyekiti wa wamiliki wa mabasi mkoani Tanga amesema, "Tunawashukuru LATRA na TRA kwa kutupatia elimu hii na tunaahidi kuendelea kutumia mfumo huu kwa kuwa una manufaa kwa wote na tunaahidi kuzifuata kanuni za usafirishaji kama ambavyo tumeelekezwa na LATRA. "

# UFAHAMU MFUMO WA VTS NA JINSI UNAVYOFANYA KAZI

Umeshawahi kusafiri na basi kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine? Katika Safari yako umeshawahi kusikia muito wa kengele ukipiga katikati ya safari? Kengele hiyo uliichukuliaje? Ulielewa maana yake na kuchukua hatua au uliiacha na kuona kuwa ni kelele za kawaida? Kengele unayoisikia ukiwa safarini kwenye basi ni kiashiria ya kwamba gari hilo limefikia au limezidisha mwendo ulioidhinishwa na Serikali yaani linaendeshwa kwa mwendokasi wa kilometa 80 kwa saa au zaidi na hivyo inahatarisha maisha yako na wengine waliopo ndani ya basi hilo.

Suala la ajali barabarani limekuwa likigharimu maisha ya Watanzania wengi hapa nchini. Wapo wanaopoteza maisha, wapo wanaopoteza viungo nakusababishiwa ulemavu wa kudumu na wapo wanaoachwa yatima kwa kupoteza wapendwa wao kwenye ajali. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakisikitishwa sana na hali hii kwa kuwa nguvu kazi ya Taifa imekuwa ikipotea na imefanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba changamoto ya ajali barabarani inapungua au kuondoka kabisa.

Katika kutafuta mwarobaini wa ajali za barabarani hasa za mabasi ya masafa marefu, mwaka 2017 Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) ilianzisha Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari ambao kwa kimombo unafahamika kama 'Vehicle Tracking System-VTS' kwa lengo la kuhakikisha kuwa magari yanapokuwa barabarani yanafuatiliwa kwa ukaribu hasa suala la mwendo kasi na mwenendo wa dereva anayeendesha gari hilo.

Akizungumzia chimbuko la kutengeneza Mfumo wa VTS, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA LATRA Mhandisi Eliud Kataraihya anasema kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo kubwa la watu kupoteza maisha kutokana na ajali barabarani. Uchunguzi wa matukio mbalimbali ya ajali ulionesha kuwa ajali ajali zenye madhara makubwa kwa binadamu husababishwa na vyombo vya usafirishaji, hususan mabasi, kuendeshwa kwa mwendo kasi. Kwahiyo, kunusuru hali hiyo, mwaka 1997 Serikali ilikuja na kifaa cha kudhibiti mwendo (speed governor) lakini kwa wakati ule haikufanikiwa sana.


Anaongeza kuwa, Serikali iliendelea kufanya jitihada za kuleta suluhisho na hivyo tafiti mbalimbali ziliendelea kufanyika na ndipo ikaonekana kwamba suala hili linaweza kukabiliwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari au kama inavyofahamika kwa jina la VTS.

Mhandisi Kataraihya anaongeza kuwa, Mfumo wa VTS umeleta manufaa makubwa kwakuwa umechangia sana kubadilisha tabia za madereva kwa sababu pindi dereva anapokuwa barabarani na chombo cha moto, anajua kwamba wapo watu wanamuona na kufuatilia mwenendo wa chombo chake, anajua mwendo anaoendesha unahifadhiwa, breki za ghafla anazokanyaga zinaonekana, kona anazopita kwa mwendo kasi anaonekana na mfumo unatuma taarifa papo hapo anapoendesha kwa mwendo kasi na hivyo basi inamfanya dereva makini azingatie kanuni za usalama barabarani.

Akielezea jinsi mfumo wa VTS unavyofanya kazi, Mhandisi Kataraihya anasema kuna kifaa cha kufuatilia mwenendo wa gari kinachofahamika kama VTD ambacho kinawekwa ndani ya gari husika. Kifaa hicho kina uwezo wa kupata mawasiliano kutoka kwenye Satelaiti zinazokisaidia kifaa kujua sehemu gari ilipo na ndani yake inatumia kadi ya simu yenye uwezo wa kutumia taarifa au data za mitandao ya simu kutuma taarifa kutoka kwenye VTD kupitia minara ya simu iliyopo karibu na kisha taarifa kutumwa kwa njia ya intaneti na kuingia kwenye seva za Mamlaka.

"Zikishaingia kwenye seva za Mamlaka tuna uwezo wa kuzichakata kwa namna mbalimbali na kuwasilisha taarifa mbalimbali ambazo nyingine atazihitaji mmiliki wa chombo husika, nyingine tunazihitaji sisi kama wadhibiti na nyingine zitahitajika na Mamlaka nyingine za Serikali na wadau wengine wa Sekta ya Usafiri Ardhini hapa

Inaendelea uk.14 >>





<< Inatoka uk.13

nchini," anafafanua Mhandisi Kataraihya.

Katika kuhakikisha kwamba Mfumo wa VTS unafanya kazi kwa ufanisi, unaleta tija iliyokusudiwa na inaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, Mhandisi Kataraihya anasema mfumo umeboreshwa ambapo kwa sasa dereva atakayeendesha chombo chake kwa mwendo kasi, mfumo unauwezo wa kutuma namba ya malipo moja kwa moja kwa dereva kwa ajili ya kulipa faini kwa kosa alilolifanya jambo ambalo kabla ya maboresho, mmiliki wa gari ndiye aliyekuwa akilipa faini hiyo kutokana na kosa alilofanya dereva, lakini kwa sasa dereva akifanya kosa la mwendo kasi ndiye atakayewajibika kupitia mfumo wa VTS. "Tumefurahi kwa maboresho tuliyoyafanya na kukamilisha na kwa sasa tupo kwenye mazungumzao na wadau ya namna gani na lini jambo hili linaanza kufanya kazi."

Mhandisi Kataraihya anaeleza maboresho mengine ya Mfumo wa VTS yanayofanyika na anasema kuwa Mamlaka inakamilisha mpango wa kufunga runinga kwenye Kituo Kikuu cha Mabasi Dodoma na Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kwa lengo la kutoa taarifa mbalimbali kwa abiria wanaosafiri kwenda maeneo mbalimbali. Vilevile Mamlaka imetengeneza programu tumizi wa Simu Janja (LATRA App) ambayo kwa sasa inapatikana kwenye simu zinazotumia mfumo wa Android zenye programu ya Play Store lakini hapo baadae itapatikana kwenye simu zinazotumia mfumo wa IoS zenye programu ya App Store.

Programu hii ya LATRA App inafanyiwa maboresho pia ili kuiwezesha kuzungumza na mfumo wa VTS kwa maana ya kwamba itafika kipindi ambapo msafiri akitaka kujua mwendo kasi wa gari alilopanda ataweza kutumia simu yake kwa kuingia kwenye LATRA App na kupata taarifa hiyo na anaweza kuitolea taarifa papo hapo alipo.

"Tumepanga kufanya maboresho ya taarifa mbalimbali ambazo wamiliki wa magari yanayofuatiliwa kupitia Mfumo wa VTS wanaweza kuona, tunaboresha taarifa ambazo wasimamizi wa magari wanaweza kuziona, kuzifanyia kazi na kuchua hatua stahiki na kwa haraka," anaeleza Mhandisi Kataraihya

Naye Afisa Mfawidhi Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari Bw. Mbwana Ndaro anasema kuwa kifaa cha ufuatiliaji wa mgari au VTD kimefungwa kwenye magari yanayotoa huduma kati ya mji na mji na kinachofanyika ni kwamba mfumo unarekodi taarifa mbalimbali ambazo zina maana tofautitofauti kulingana na mahitaji na kikubwa dhumuni hasa la mfumo wa VTS ni kuhakikisha kwamba madereva wanaendesha vyombo vya moto kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani ambayo kikomo ni Kilometa 80 kwa saa na endapo ikitokea dereva anavuka mwendo kasi unaotakiwa, mfumo unatuma taarifa papo hapo nasi tunachukua hatua stahiki kwa wakati.

"Baada ya kuona gari linaenda mwendo kasi zaidi ya inaotakiwa, tunaangalia ni gari gani na kisha tunampigia mmiliki ili kumuarifu kuhusu dereva wa chombo chake anavyoendesha kwa mwendokasi, tunamwambia mpaka mahali gari lilipo kwa wakati huo na anaendesha kwa mwendo kasi huo kwa mara ngapi. Wakati mmiliki anaendelea na dereva wake, sisi tunawataarifa watumishi wenzetu waliopo eneo ambalo gari husika linaelekea na tunatuma taarifa zote ili achukuliwe hatua," anafafanua Bw. Ndaro.

Bw. Ndaro anaongeza kuwa LATRA inashirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ambapo baada kumuona dereva bado anaendesha mwendo hatarishi, hupiga simu kwa Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa (RTO), Kanda (ZTO) na Wilaya (DTO) na kuwaarifu kuhusu mwendo kasi wa gari husika ili nao wasimamishe basi na waweze kuchukua hatua mapema zaidi kwa kuwa mwendo huo unaweza kusababisha ajali na kuondoa uhai wa abiria waliopo ndani ya basi husika. Kwahiyo muunganiko wa LATRA, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na wamiliki ambao wamekuwa wakitoa ushirikiano wa hali ya juu, unaifanya kazi hii ya kufuatilia mienendo ya magari kuwa rahisi na hivyo kusaidia kupunguza changamoto ya ajali hapa nchini.

"Sisi kama Mamlaka tunashirikiana na kufanya kazi kwa ukaribu na Jeshi la Polisi

Inaendelea uk.15 >>

<< Inatoka uk.14

Kikosi cha Usalama Barabarani na kwa umuhimu wake, Mamlaka imewapatia akaunti za Mfumo wa VTS RTO na DTO ili kuweza kuyafuatilia mabasi husika kwa sababu pia tunatumia Sheria ya Usalama Barabarani katika kutoa adhabu kwa madereva ambao wanakiuka taratibu zilizowekwa hasa ya kuendesha kwa mwendo hatarishi," amefafanua Bw. Ndaro.

Akielezea faida za Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) Bw. Ndaro anasema umeisaidia sana Serikali kupunguza ajali nchini kwa kuhakikisha kwamba madereva wanaendesha gari kwa kuzingatia mwendo ulioainishwa kwenye Sheria ya Usalama Barabarani ambayo kikomo chake ni Kilometa 80 kwa saa.

Kwa wamiliki pia imewasaidia kupunguza gharama za uendeshaji ukizingatia kabla ya mfumo wasafirishaji walikuwa wanatumia mafuta mengi lakini uwepo wa mfumo huu wa VTS imethibitika kwamba utumiaji wa mafuta umekuwa ni mdogo na hivyo kuleta afueni kwa wamiliki wa magari na pia wana uwezo wa kufuatilia gari na dereva husika akiwa barabarani na hivyo kumsaidia kumdhibiti dereva wake.

Kwa upande wa abiria pia unamsaidia kufahamu kile kinachoendelea kwenye gari hasa kupitia kengele (alarm) ambayo inatoa sauti pindi dereva anapoendesha gari kwa mwendo hatarishi na hivyo anaweza kuchukua hatua kwa kumuarifu dereva kupunguza mwendo au kwa kupiga simu LATRA au kwa Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi.

SP. Deus Sokoni ni Mrakibu Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, nae anasema VTS inaunganishwa na mtandao wa GPS lengo likiwa ni kufuatilia na kujua mwendo wa gari barabarani na mwenendo wa dereva katika uendeshaji wake kwa maana kuna wakati mwingine dereva yupo barabarani lakini anafanya vitendo ambavyo vinaenda kinyume na Sheria ya Usalama Barabarani na hivyo anaweza kuhatarisha usalama wa abiria aliowabeba ndani ya gari hiyo na haya yote yanatambulika kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari kwa maana ya VTS.

Vilevile SP. Sokoni anaongeza kuwa VTD ni kifaa muhimu sana katika usimamizi wa Sheria, mathalani kwa dereva anayevunja Sheria kwa kukimbiza gari zaidi ya mwendo wa Kilometa 80 kwa saa na akabainishwa na mfumo wa VTS, Jeshi la Polisi lina Mamlaka ya kutumia ushahidi uliopatikana kwenye Mfumo huo na kuutumia mahakamani au kuchukua hatua zozote zile za kisheria zinazostahili ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na barabara zilizo salama zaidi.

SP. Sokoni anabainisha kuwa utendaji kazi wa Mfumo wa VTS unategemea sana ushirikiano na anaeleza kuwa LATRA na Jeshi la Polisi ni taasisi za Serikali hivyo wamekuwa wakifanya kazi bega kwa bega kuhakikisha kuna usalama kwenye sekta ya usafirishaji, "Tumepewa jukumu la kusimamia usalama wa watumiaji wa barabara na kila mtu kwa nafasi yake, LATRA kama mdhibiti wa Usafiri Ardhini anao wajibu wa kuhakikisha wasafirishaji wanafuata Sheria zilizopo na sisi Jeshi la Polisi ambalo ni msimamaizi wa Sheria ni jukumu letu kuhakikisha kuna usalama wa raia na mali zao na hivyo mfumo huu wa VTS ungebaki LATRA pekee usingukuwa na tija. Tunaishukuru Mamlaka kwa kuona kuna umuhimu wa kutushirikisha sisi Jeshi la Polisi ili kuhakikisha lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa VTS linatimia,"

SP. Sokoni anaongeza kuwa, LATRA ilitoa mafunzo kwa askari wa usalama barabarani hasa namna ya kutumia mfumo huo na jinsi ya kumbaini dereva na vilevile LATRA imefunga mfumo wa VTS kwenye Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ili kuweza kufanya ufuatiliaji kwa pamoja kudhibiti madereva wanaokiuka Sheria na masharti ya leseni ya usafirishaji inayomtaka kuzingatia na kuheshimu Sheria za Usalama Barabarani, "Tunafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha barabara zinakuwa salama kwa kutokuwa na ajali, kuona madereva wanaheshimu na kufuata Sheria zilizopo yaani Sheria ya Usalama Barabarani na ile ya Usafirishaji."

Akielezea namna mfumo wa VTS ulivyosaidia kupunguza ajali barabarani, SP Sokoni anasema



***Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA alipotembelea kituo cha kufuatilia mwenendo wa magari (VTS Center).***

Inaendelea uk.16 >>




<< Inatoka uk.15

kuwa kwa sasa madereva wanajua kwamba wanafuatiliwa wakiwa barabarani na hivyo inawalazimu kufuata Sheria jambo ambalo limeleta nafuu ya kupunguza ajali ukilinganisha na miaka ya nyuma kabla ya mfumo huo. “Mwaka jana tulikuwa na zaidi ya ajali 117 lakini kufikia mwezi Novemba 2022 kuna ajali 102 kwahiyo ajali hasa zinazotokana na mwendo kasi wa mabasi zimepungua sana na hii yote inachangiwa na mfumo huu wa VTS.”

Hivi karibuni Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC) ilitembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ili kujionea namna Mfumo huo unavyofanya kazi. Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Naghenjwa Kaboyoka (MB) anasema, “Wenzetu wa LATRA wamepiga hatua kubwa sana upande wa teknolojia hasa ukizingatia uwepo wa Mfumo huu wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali za barabarani. Tumeona mfumo unavyoweza kufuatilia basi na kama litakuwa limezidisha mwendo unaotakiwa mfumo unawatumia taarifa na wao wanachukua hatua dhidi ya gari husika.”

Aidha, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka, akiungana na wabunge wengine wameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafirishaji Ardhini (LATRA) kwa maendeleo ya teknolojia ambayo wameyafikia kwani ni msaada mkubwa kwa Taifa, “Hatukutegemea tuone jinsi ambavyo wamefanya maboresho makubwa sana kiasi hiki na jinsi ambavyo sheria zetu kinzani zikirekebishwa, Tutaweza sana kupunguza mambo ya ajali barabarani, Tunaona mfumo unavyoweza kufuatilia basi mpaka linalokwenda mbio, linalo kiuka misingi.”

Naye Mhe. Geoffrey Mwambe (MB) Mjumbe wa PAC anesema kuwa, “Kwa kweli tumefurahi sana kuona wenzetu wa LATRA walivyopiga hatua kubwa kwa kutengeneza mifumo ya usimamizi wa usafirishaji wa ardhini hasa mfumo huu wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari na tumeona kuwa mfumo huu ni wezeshi wa kupunguza changamoto za ajali barabarani (VTS).”

Wakati huohuo, Mhe. Aida J. Kanani (MB) Mjumbe wa PAC anaeleza kuwa, “Mfumo huu wa VTS ni mzuri sana, LATRA wameshaanza na magari hayo ya abiria lakini itakuwa vizuri zaidi mpaka kwa magari binafsi ili tuweze kufikia lengo la kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la ajali barabarani kwa sababu ajali za barabarani zinahusisha magari ya aina yote yakiwemo na ya Serikali kwa hiyo nafikiri ni vema ifikie mahali kwamba kila gari itakayoingia nchini na kutumika barabarani iunganishwe na Mfumo wa VTS na hii itasaidia sana suala la ufuatiliaji na udhibiti wa ajali.”

Kwa upande mwingine, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) Bw. Abdallah Kiongozi anasema VTS ni Mfumo mzuri kwa sababu unawawezesha wamiliki kufuatilia gari likiwa kwenye safari ikiwemo suala la mwendo na kama mmiliki unaweza kumuonya dereva wako kupunguza mwendo hatarishi, “VTS ina mambo mengi mazuri kama vile kusaidia utunzaji wa chombo, unafuu wa matumizi ya mafuta, matumizi mazuri ya breki, utunzaji mzuri wa vipuri vya gari pamoja na kupunguza tatizo la ajali barabarani kwakuwa VTS inadhibiti na dereva anajua kuwa kuna VTS inayomfuatilia na inamuonya na hivyo inamfanya azingatie mwendo akiwa barabarani.”

Naye Anna Zacharia ni abiria na anaeleza kuwa, “tunaishukuru LATRA kwa kutuwekea mfumo

Inaendelea uk.17 >>

## UFAHAMU MFUMO WA VTS NA JINSI UNAVYOFANYA KAZI

<< Inatoka uk.16

huu na kutupa elimu, na sasa sisi kama abiria tunaelewa kwamba tukisikia kengele ndani ya basi tukiwa safarini tunajua kuwa dereva anaendesha mwendo wa kasi na hivyo tunawajibika kumwambia apunguze mwendo la sivyo tunapiga simu LATRA au Jeshi la Polisi maana tukikaa kimya inaweza kutokea ajali na tukapoteza maisha".

Hakika Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) umesaidia sana kupunguza changamoto ya ajali ambazo zimekuwa zikipoteza uhai wa watanzania wengi hapa nchini. Kwa madereva ambao bado wanakwenda kinyume na Sheria ya Usalama Barababari na Sheria ya Usafirishaji hasa ya inayowataka kuzingatia mwendo ulioidhinishwa na Serikali ambao ni Kilometa 80 kwa saa, yawapasa wabadilike kwakuwa Serikali imewekeza katika teknolojia na imeuleta mfumo wa VTS ili kuhakikisha sekta ya Usafiri Ardhini inakuwa salama. Mfumo wa VTS unafuatilia mabasi ya masafa marefu na treni za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA).

Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tayari iko katika taratibu za kuboresha mfumo wa VTS ili uwe na uwezo wa kufanya kazi ya kudhibiti mwendo (Speed Governors) ili kuendelea kudhibiti mwendo kasi unaosababisha matukio ya ajali zenye madhara makubwa kwa binadamu. Pia Mamlaka imekwishaanza kuthibitisha madereva ili kuhakikisha ni madereva makini tu wanaruhusiwa kuendesha vyombo vya vinavyotoa huduma za usafirishaji kibiashara.




*CPA Habibu Suluo (mwenye tai nyekundu), Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akizungumzia kufungiwa kwa watoa huduma wa VTS jijini Dar es Salaam.*

## LATRA YAWASIMAMISHA UTRACK AFRICA LTD NA EASY TRACK SOLUTION JV RJ MOTCHAND LTD

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewasimamisha watoa huduma wawili wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi ambao vifaa vyao vimebainika kuchezewa. Watoa huduma hao ni Utrack Africa Ltd na Easy Track Solution JV RJ Motchand Ltd.

Akizungumza na waandishi wa habari Aprili 11, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amesema kampuni hizo zilifanyiwa tathmini kwa mujibu wa Mkataba ambapo Mamlaka ilibaini mapungufu yasiyovumilika.

"Kampuni hizi mbili ndizo zilizofunga kifaa cha kufuatilia mwenendo wa magari (VTD) kwenye mabasi 27 ambayo yamefungiwa kwa mwezi Machi, 2023. Kwa sasa zinatakiwa kurekebisha kasoro zilizobainika kwenye mabasi yaliyofungiwa na wakikamilisha watarudishwa kuendelea na utoaji wa huduma ya kufunga vifaa vipya,"ameeleza CPA Suluo.

LATRA iliingia Mkataba na Watoa Huduma watano (5) ambao ni kampuni zilizochaguliwa kwa mchakato wa zabuni wa kufunga vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari (VTDs) ambao ni Fleet Truck, Tera Technologies, Easy Truck, Utruck na ICTPack.

> **"Kampuni hizi mbili ndizo zilizofunga kifaa cha kufuatilia mwenendo wa magari (VTD) kwenye mabasi 27 ambayo yamefungiwa kwa mwezi Machi, 2023.**

# MABASI 49 YAFUNGIWA NDANI YA MIEZI 3

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa vipindi tofauti imekuwa ikifungia kwa muda baadhi ya magari kutoa huduma ya kusafirisha abiria kutokana na kukiuka masharti ya leseni zao za usafirishaji, kosa lililojitokeza zaidi ni kuchezea Mfumo wa kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

Kwa nyakati tofauti Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo na Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara Bw. Johansen Kahatano wamebainisha zaidi ya mabasi 49 yamefungiwa kutoa huduma kwa mwezi Januari hadi Machi 2023, kwa kukiuka masharti ya leseni ambayo ni kwa mujibu wa Sheria.

CPA Suluo amesema uamuzi huo umefanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Kanuni ya 27(1)(c) na (d) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020.

"Hatua hii ni kutokana na vitendo vya kuingilia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kusababisha mfumo kutotuma taarifa kabisa ama kutuma taarifa kwa kurukaruka (skipping). Hapa kuna baadhi ya mabasi ambayo baada ya wataalamu wa Mamlaka kufanya uchunguzi, waligundua betri za vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTDs) zimeharibiwa na mifumo yake ya umeme kubadilishwa," amefafanua CPA Suluo.

Vilevile amesema kuwa, kuna mabasi ambayo yamekutwa yakiwa na mfumo wenye swichi inayotumiwa na dereva kuzima na kuwasha kifaa hicho (VTD) na hatari zaidi ni kwamba yapo mabasi ambayo yamebadilishwa mfumo (software) na kutuma taarifa za uongo kwenye kituo cha ufuatiliaji wa mwenendo wa magari.

"Ninawasihi madereva na wasafirishaji wote kuacha tabia hii mara moja na wafahamu kuwa mfumo wa VTS una uwezo wa kutoa taarifa kwa Mamlaka iwapo utaingiliwa au kuharibiwa, tutaendelea kutoa adhabu kwa wale wote wanaofanya vitendo hivi ambavyo havikubaliki na vinahatarisha maisha ya watanzania wanasafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine," amesisitiza CPA Suluo.

Aidha, CPA Suluo ameeleza kuwa, kitendo cha kuingilia Mfumo wa VTS ni ukiukwaji wa Kanuni ya 51(a) na (b) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020 ambapo Kanuni ya 51(a) inamtaka mmiliki (mwenye leseni) ahakikishe basi lake limefungwa kifaa cha kufuatilia gari (installed with VTD), kiwe kinafanyakazi vyema (working properly), kinafanyiwa marekebisho (maintained), kinakingwa na mazingira hatarishi (protected against hazardous conditions) na hakichezewi (tempering).

Kwa upande wake Bw. Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara amebainisha kuwa LATRA imekubaliana na Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za Kisheria wamiliki wa mabasi kwa kufungia leseni lakini pia madereva wa basi husika nao wachukuliwe hatua za Kisheria kwa uvunjifu wa Sheria za Usalama Barabarani.

"Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tunadhibiti kila upande ili kuhakikisha kwamba madereva wana sehemu yao ya kuwajibika lakini pia wamiliki wa magari wana sehemu yao ya kuwajibika," ameongeza Bw. Kahatano.

Bw. Kahatano amewakumbusha wasafirishaji wenye nia njema na mfumo wa VTS kuwa, wanaweza kufuatilia mabasi yao kupitia simu zao za mkononi ili waweze kuangalia mwenendo mzima wa mabasi yao na kuona taarifa zote wakati mabasi yakiwa safarini kwani wamepatiwa akaunti zao ambazo zimeunganishwa na mfumo wa VTS moja kwa moja.

Inapotokea msafirishaji anaona maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka hayajamridhisha, Sheria inamtaka msafirishaji kupinga maamuzi hayo kwa hoja na kuna Jopo la Mapitio (Review Panel) ya Bodi itafanya kazi yake na kutoa maamuzi, Na endapo msafirishaji hajaridhika na maamuzi ya Jopo, basi hatua inayofuata ni kwenda kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal).




*CPA Habibu Suluo (mwenye tai nyekundu), Mkurugenzi Mkuu wa LATRA pamoja na Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani SACP Ramadhani Ng'anzi wakitangaza kufungiwa kwa mabasi hayo*

# LATRA YATANGAZA NAULI MPYA MABASI YAENDAYO HARAKA, TEKSI MTANDAO

> **“Nipende kuwakumbusha watoa huduma wa haya mabasi yaendayo haraka kuwa, nauli wanazopaswa kutoza ni hizi tulizozitangaza.**



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza nauli mpya za Teksi Mtandao, Pikipiki Mtandao na Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) zitakazotumika nchini siku 14 kuanzia sasa. Nauli hizo zimetangazwa Januari 3, 2023 na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo jijini Dodoma.

Akizungumza na Wanahabari, CPA Suluo amesema, tangazo hilo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, ambapo LATRA imepewa jukumu la kupanga nauli za vyombo vinavyotoa huduma za usafiri ardhini kibiashara.

Nauli mpya kwa Mabasi Yaendayo Haraka ni shilingi 750 kutoka shilingi 650 iliyokuwa awali kwa njia kuu na shilingi 500 kutoka shilingi 400 kwa njia mlisho sawa na ongezeko la shilingi 100, abiria watakaounganisha njia kuu na njia mlisho watalipia shilingi 900 na kwa njia ya Kimara hadi Kibaha watalipia shilingi 700.

CPA Suluo amefafanua kuwa, teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne (4) kiwango cha chini kitakuwa shilingi 3,000 na kiwango cha juu kitakuwa shilingi 4,000 kwa safari isiyozidi kilomita moja. Aidha, nauli ya kuanzia safari ni shilingi 500 hadi 1,000, nauli kwa kilomita ni shilingi 800 hadi 1,000, nauli kwa dakika ni shilingi 80 hadi 100.

Vilevile, teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi sita (6) nauli ni shilingi 4000 hadi 5000 kwa safari isiyozidi kilomita moja. Nauli ya kuanzia safari ni shilingi 800 hadi 1,300, nauli kwa kilomita ni shilingi 1,000 hadi 1,200, nauli kwa dakika ni shilingi 80 hadi 150.

Kwa upande wa pikipiki mtandao, nauli mpya kwa pikipiki zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wawili (2) ni shilingi 1,000 hadi 1,500, nauli ya kuanzia safari ni shilingi 250 hadi 350, nauli kwa kilomita ni shilingi 300 hadi 400, nauli kwa dakika ni shilingi 50 hadi 70.

Na kwa pikipiki zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi watatu (3) nauli ni shilingi 2,000 hadi 2,500 kwa safari isiyozidi kilomita moja, nauli ya kuanzia safari ni shilingi 350 hadi 500, nauli kwa kilomita ni shilingi 500 hadi 600, nauli kwa dakika ni shilingi 70 hadi 90.

Aidha CPA Suluo amesisitiza kuwa, nauli zitakazotumika katika mabasi yaendayo haraka ni zile zilizotangazwa na Mamlaka na kuwa mfumo wa utoaji tiketi utakaokubalika ni wa kielektroni au kadi ambazo zinakubalika na watoa huduma.

“Nipende kuwakumbusha watoa huduma wa haya mabasi yaendayo haraka kuwa, nauli wanazopaswa kutoza ni hizi tulizozitangaza, na tiketi halali ni zile zinazotolewa kwa njia ya kielektroni au zile kadi ambazo za kusafiria zinakubalika,” amesema CPA Suluo.

# LATRA YAKABIDHI VIFAA VYA VTS KWA JESHI LA POLISI

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Prof. Ahmed Mohammed Ame, amekabidhi vifaa vya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ikiwemo runinga mbili, kompyuta mbili pamoja na kompyuta mpakato mbili kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ili kudhibiti hali ya usalama kwa vyombo vya moto viwapo safarini na kupunguza ajali nchini.

Makabidhiano hayo yamefanyika katika ofisi za LATRA jijini Dar es Salaam Ijumaa Machi 31, 2023. Akizungumza na wadau mbalimbali waliohudhuria makabidhiano hayo, Prof. Ame amesema kuwa lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuongeza ushirikiano uliopo kati ya LATRA na Jeshi la Polisi na kudhibiti ajali ambazo hivi karibuni zimekuwa zikijitokeza.

"Lengo letu ni kuongeza ushirikiano zaidi na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ili kufuatilia mwenendo wa mabasi yawapo safarini, kama mtakuwa wafuatiliaji wazuri, usalama barabarani umekuwa si mzuri na hivi karibuni kumetokea ajali nyingi barabarani zinazo gharimu maisha ya watu wengi na kuharibika kwa mali nyingi," amesema Prof. Ame.

Aidha Prof. Ame ameeleza kuwa moja ya faida ya vifaa ambavyo LATRA imewakabidhi Jeshi la Polisi ni pamoja na kuwawezesha kufatilia mwenendo wa magari ya abiria yawapo safarini kupitia mfumo wa VTS.

"Vifaa hivi vitawawezesha Jeshi la polisi kikosi cha usalama barabarani kufatilia mwenendo wa mabasi barabarani hasa haya mabasi yanayokwenda masafa marefu (mabasi yanayokwenda mikoani na nje ya nchi) ili kupunguza ajali za barabarani nchini," ameeleza Prof. Ame.

Kwa upande wake, CPA Habibu Suluo Mkurugenzi Mkuu LATRA amekemea madereva na wamiliki wa mabasi ambao wamekuwa wakichezea vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari (VTD) hali inayoongeza hatari ya kupata ajali wakiwa safarini, na kusisitiza hatua za kisheria kuchukuliwa.

"Kiukweli mtu anapochezea vifaa hivi vya kufuatilia mwenendo wa magari maana yake anahatarisha kwa makusudi maisha ya watanzania, hivyo tunatoa onyo kwa madereva na wamiliki wa mabasi waache kuchezea mfumo wa VTS ikiwa wakikiuka watachukuliwa hatua za Sheria, wapo ambao tumewafungia hadi siku 30," amesema CPA Suluo.

Naye mwakilishi wa Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani ACP Meloe Buzema ameishukuru LATRA kwa kukabidhi vifaa hivyo ambavyo vitaongeza ufanisi katika udhibiti wa mwenendo wa magari ya abiria nchini.

"Kuwepo kwa teknolojia ya mfumo wa VTS kumesaidia kupunguza viwango vya ajali ukilinganisha na kipindi cha nyuma. Naamini baada ya kupokea vifaa hivii kutakuwa na mabadiliko makubwa katika kudhibiti ajali za barabarani," ameeleza ACP Buzema.

LATRA imekuwa na desturi ya kushirikiana na wadau mbalimbali wa Usafiri Ardhini wakiwemo jeshi la polisi kikosi cha Usalama Barabarani ili kuboresha huduma za Usafiri nchini ikwa ni pamoja na kupunguza ajali,




***Prof. Ahmed Mohammed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA akikabidhi vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.***



***Bw. Daniel Chilongani, Afisa Usajili na uthibitishaji wa Madereva Msaidizi (LATRA) akiwasaidia madereva waliojitokeza kusajiliwa na kufanyiwa ithibati.***

# LATRA KUONGEZA KASI YA USAJILI WA MADEREVA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepanga kuongeza kasi zaidi ya usajili wa madereva ili kupunguza vifo na hasara zitokanazo na ajali za barabarani.

Makakati huo umeelezwa na Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara baada ya kikao cha kupokea taarifa ya uchunguzi wa ajali za magari zilizotokea Wilayani Kongwa, Mkoani Dodoma na Wilayani Korogwe, Mkoani Tanga kilichofanyika katika ofisi za LATRA mkoa wa Dar es Salaam Februari 16, 2023.

"Tumeweza kupata baadhi ya sababu zilizosababisha ajali lakini pia tumepata mapendekezo ikiwemo kuongeza kasi katika usajili wa madereva hasa kwa mabasi makubwa na mabasi madogo ya kukodi na sisi kama Mamlaka tumekubaliana mpaka kufikia tarehe 28 Februari 2023 madereva wa mabasi madogo ya kukodi wote wawe wameshasajiliwa," amesema Bw. Kahatano.

Kwa upande wake msimamizi wa uchunguzi wa ajali hizo Bw. Jonathan Mmari amesema ajali zote mbili zilikuwa na sababu zinazoweza kuzuilika hivyo zimetokea kwa uzembe katika safari hizo.

"Sababu za ajali zilikuwa zinazuilika ikiwemo kulipita gari iliyopo mbele mahali ambapo haijaruhusiwa, madereva kutokupata muda mzuri wa kupumzika baada ya safari, mwendo kasi uliopitiliza, abiria kutofunga mkanda wakati wa safari na kuzidisha uzito kwenye gari, hivyo mapendekezo yetu ni magari ya mizigo yafungwe vidhibiti mwendo (VTS), lakini pia madereva wote wapate mafunzo na wasajiliwe LATRA," amesema Bw. Mmari.

Kwa upande wake Afisa Viwango kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Mha. Prosper Godfrey, ameelezea jukumu la TBS katika kuzuia ajali za barabarani, "Sisi kama TBS tuna kazi ya kuangalia viwango vya magari kama yanafaa kutumika barabarani, tuna kazi ya kuthibitisha magari ambayo yanafanyiwa maboresho kama vile kuongezwa urefu na uzito na kuyapa kibali cha kuendelea kusafirisha, kwa ajali iliyotokea Kongwa lile lori liliongezewa uzito kutoka tani 4 hadi 10 ambapo haikuwa sahihi na wala haikuthibitishwa na TBS."

Akiongelea Mitaala ya kujifunzia madereva, Kamanda wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Ramadhani Ng'anzi amesema mitaala ya shule za madereva iangaliwe na kufanyiwa maboresho ili kuweza kupata madereva ambao wana uweledi.

"Mitaala ya vyuo vya udereva iangaliwe vizuri ili kuweza kutoa mafunzo ambayo yatawafanya madereva kufuata Sheria na Kanuni katika kazi zao hivyo inaweza kupunguza ajali za barabarani, tunaamini chuo kikiwa bora kitatoa madereva bora pia," amesema SACP Ng'anzi.

Usalama wa Barabarani na safari sio jukumu la Mamlaka za Serikali peke yake bali ni jukumu la kila mmoja, ni wajibu wa dereva kuhakikisha kuwa anaendesha chombo kilicho salama kwa matumizi na kwa mwendo ulio salama, ni jukumu la abiria kumkumbusha dereva wanapoona mwendo ni hatarishi, jali maisha yako na ya mwenzako.

# MADEREVA 15 WASITISHIWA LESENI

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limesitisha leseni za madereva 15 wa mabasi ya masafa marefu waliohusika kuharibu Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) ili mabasi yao yakimbie pasipo kuonekana kwa kipindi cha mwezi Machi, 2023.

Hayo yamezungumzwa na Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani SACP Ramadhani Ng'anzi kwenye kikao na waandishi wa habari kilichofanyika Aprili 11, 2023 katika ofisi za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Dar es Salaam.

SACP Ng'anzi amesema kuwa suala la udhibiti usalama barabarani ni endelevu na Jeshi la Polisi halitovumilia kuona maisha ya watanzania yanawekwa rehani na madereva wasiofuata Sheria.

"Tulifanya ukaguzi wa Mfumo wa VTS na tuligundua mfumo huo umechezewa na sisi tukachukua hatua ya kuwafungia madereva na baadhi yao kuwafutia kabisa leseni zao. Tutaendelea kudhibiti mienendo ya madereva na niwasihi madereva wote kufuata Sheria za Usalama Barabani ikiwemo kuendesha basi kwa mwendo wa Kilometa 80 kwa saa," amesisitiza SACP Ng'anzi.

Naye Mkurugenzi Mkuu LATRA, CPA Habibu Suluo amewakumbusha wamiliki na madereva wote wa vyombo vya moto kibiashara kuhakikisha wanakamilisha usajili wa madereva kupitia https://rrims.latra.go.tz/ ifikapo Aprili 30, 2023 kama ilivyotangazwa hapo awali.

"Kwa mujibu wa masharti ya leseni za kutoa huduma ya usafirishaji, wamiliki wote wa vyombo vya usafiri kibiashara wanatakiwa kuwa na madereva ambao wamesajiliwa na kuthibitishwa. Ili kusajiliwa, dereva anatakiwa kuwa na leseni hai ya udereva, cheti cha mafunzo ya udereva na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)," amefafanua CPA Suluo.

> **"Kwa mujibu wa masharti ya leseni za kutoa huduma ya usafirishaji, wamiliki wote wa vyombo vya usafiri kibiashara wanatakiwa kuwa na madereva ambao wamesajiliwa na kuthibitishwa**




***SACP Ramadhani Ng'anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sababu ya kufungia leseni za madereva.***

# WAONGOZA WATALII NCHINI WATAKIWA KUWA NA LESENI HAI YA LATRA



***Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA akizungumza na waongoza watalii jijini Arusha.***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa wito kwa waongoza watalii nchini kuwa na Leseni hai ya usafirishaji abiria ambayo ni maalumu kwa magari ya watalii, ili kuepusha usumbufu kwa madereva na watalii kwa jumla.

Wito huo umetolewa na Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA kwenye mkutano wa mafunzo kwa waongoza watalii nchini ulioandaliwa na LATRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha. Mkutano huo umefanyika katika ukumbi wa Mt. Carolus uliopo Jijini Arusha April 20, 2023.

Akizungumza baada ya mkutano huo Bw. Kahatano amesema, kwa kuwa tayari waongazaji watalii wamefahamu umuhimu wa kuwa na leseni ya LATRA, ni vyema wakajitokeza wote kukata leseni hiyo ili kuboresha Sekta ya Utalii nchini.

"Kimsingi Waongozaji Watalii wamefahamu uhusiano uliopo baina yetu hivyo nawasihi wawe na leseni hai za LATRA. Ni vizuri wakajituma wenyewe na kukata leseni hizo ili kuepusha usumbufu wawapo safarini au kwa watalii kwa jumla, kwa maana tumewaelekeza pia jinsi ya kuangalia kama leseni zao zipo hai kwa njia ya mtandao," amesema Bw. Kahatano.

Vilevile amewahimiza wamiliki wa vyombo vya usafiri kibiashara kutumia huduma za LATRA ambazo zinapatikana kwa njia ya mtandao na kuepuka kuwatumia watu wa kati "VISHOKA" ambao wanafanya huduma za LATRA zionekane ni za gharama zaidi kuliko uhalisia.

"Huduma za LATRA zinatolewa kwa njia ya mtandao, mtu anaweza kuomba leseni mpaka kupatiwa namba ya malipo akiwa nyumbani kwake au ofisini, hivyo akawa na safari moja tu ya kufika ofisini kwetu na kuchukua leseni yake. Badala ya kutumia watu wa kati "VISHOKA" wanaweza kujihudumia wenyewe mahali walipo na kupunguza gharama za maisha," ameongeza Bw. Kahatano.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw. Misaille Musa ameitaka LATRA kukaa pamoja na Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ili kujadili na kupata ufumbuzi wa taka zinazozalishwa na mabasi pamoja na daladala katika Jiji la Arusha.

Akiyazungumzia mafunzo hayo waliyopatiwa Bi. Elizabeth Ayo, Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Wanawake Tanzania (TAWTO) amesema anaamini tasnia ya Utalii nchini inakwenda kubadilika kama mapendekezo yakifanyiwa kazi na kila mmoja akitimiza wajibu wake.

Mkutano huo ulioandaliwa na LATRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa umehudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo Jeshi la Polisi, Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na waongoza watalii ambao ndio waliopatiwa mafunzo.



***Picha na Micato Safaris***



*Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA, baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti na wafanyakazi wa TRC walipotembelea mradi wa SGR.*

# BODI YA WAKURUGENZI LATRA YATEMBELEA MRADI WA SGR

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imefanya ziara katika mradi wa maendeleo ya Reli ya Kisasa (SGR) kipande kinachoanzia Dar es salaam mpaka Morogoro.

Katika ziara hiyo, Bodi ya Wakurugenzi imetembelea sehemu mbalimbali za mradi huo ikiwemo chumba maalum chenye mitambo ya kuongoza safari za treni zinazopita katika kipande cha Dar es Salaam mpaka Morogoro na Morogoro mpaka Makutupora pia imetembelea njia inayopita treni kuanzia stesheni ya Reli ya Kisasa katika jengo la Tanzanite.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA amesema mradi wa SGR umepiga hatua kubwa na imeongeza hali ya usalama pindi itakapoanza kutumika.

"Maendeleo ya SGR yamepiga hatua kubwa sana na kufikia mahala pazuri ikiwemo kuwepo kwa mifumo ya kisasa ya TEHAMA inayoongoza safari za treni popote pale inapopita, mfumo huu utasaidia na kuimarisha usalama katika njia za treni ya kisasa kwa kuonesha makosa ya kibinadamu," amesema Prof. Ame.

Naye Bw. Senzige Kisenge, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) amesema TRC imejikita katika kuboresha utendaji kazi wa reli ya kisasa kwa kutoa mafunzo jinsi ya kuongoza mifumo iliyowekwa kwa ajili ya kuongoza safari za reli.

"Yapo mafunzo yanayoendelea kutolewa hapa Dar es salaam ambayo yanayotolewa na mkandarasi aliyejenga mifumo hiyo ya kuongoza safari za treni ikiwemo mifumo inayohusu umeme na mawasiliano, mafunzo mengine yanaendelea kufanyika nchini Korea kwa kuwapeleka watu kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kuendesha mifumo hiyo," ameeleza Bw. Kisenge.

Uwepo wa Reli ya Kisasa na kuanza kufanya kazi itasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa muda na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi, mwananchi anaweza kutumia muda mfupi zaidi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine, hivyo inaokoa muda ambao angeutumia kwa safari, kwa mfano safari ya Morogoro hadi Dar es Salaam ingemlazimu mwananchi kutumia hadi saa nne kwa gari lakini atatumia saa moja tu kwa treni ya SGR.

# LATRA YAONGEZA SIKU 90 KWA MADEREVA KUJISAJILI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeongeza muda wa siku 90 kwa madereva wa vyombo vya moto kibiashara kujitokeza kwa hiari ili kusajiliwa na kufanyiwa ithibati.

Akizungumza na vyombo vya habari katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara amesema ongezeko la siku hizo ni kutokana na sababu mbalimbali zilizowafanya baadhi ya madereva kushindwa kujisajili kwa wakati uliopangwa hapo awali.

"Tumegundua sababu mbalimbali zilizofanya madereva washindwe kujitokeza kujisajili, kama vile uhitaji wa dereva kufanyiwa vipimo vya afya kama moja ya vipengele muhimu, na madereva kutopita katika shule rasmi za kujifunzia udereva, hivyo kwa kuzingatia hilo tumeongeza muda wa kuwasajili madereva kwa miezi mitatu (3) zaidi mpaka Julai 31 mwaka huu," amesema Bw. Kahatano.

Akiongelea faida za madereva kusajiliwa, Bw. Kahatano amesema usajili wa madereva utafanya fani ya udereva kutambulika kama taaluma rasmi kama zilivyo taaluma nyingine, pia kuwaongezea madereva wigo wa ajira katika Jumuiya mbalimbali ambazo Tanzania ni mwanachama.

"Usajili wa madereva utafanya fani ya udereva kufahamika rasmi kama taaluma nyingine, pia nchi yetu ipo kwenye Jumuiya mbalimbali kama vile SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa usajili huu madereva wanakuwa wamekidhi kupata uhalali wa kupata ajra katika nchi yoyote ambayo nchi yetu ni mwanachama, pia tunaweza kutambua katika muda fulani ni dereva gani anaendesha chombo kupitia kifaa cha i-button," ameongeza Bw. Kahatano.

Aidha Bw. kahatano amesema kuwa, kuanzia Mei 1, 2023 magari yanaweza kusafirisha abiria kuanzia saa 9 na saa 10 alfajiri hivyo kwa wasafirishaji wenye uhitaji wanaweza kuomba ratiba ya njia mbalimbali ili kuanza safari hizo.



*Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara, pamoja na SACP Ramadhani Ng'anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuongeza siku za kusajili madereva kwa hiari.*

"Tumefanya majaribio kwenye njia baadhi ili kuangalia namna usafirishaji utakavyokuwa na namna ya kudhibiti kwa kusafirisha abiria kuanzia saa 11 alfajiri, baada ya kujiridhisha na majaribiio hayo kuanzia tarehe 1 Mei, 2023 Mamlaka itaanza kutoa ratiba za kuanza safari saa 9.00 na 10.00 usiku kwa watoa huduma wenye kuhitaji, hata hivyo, madereva wa magari haya watapaswa kuwa wamesajiliwa na wanatumia kifaa maalum cha kumtambua dereva anayeendesha gari (i-button)," amesema Bw. Kahatano.

Naye Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani SACP Ramadhani Ng'anzi amewahimiza wamiliki wa shule za madereva kufuata vigezo na masharti yaliyowekwa ili kuzalisha madereva walio bora.

"Tumefungia shule nyingi za udereva kutokana na kutokidhi vigezo mbalimbali, hivyo niwahimize kufuata masharti yaliyowekwa ili waweze kufunguliwa, shule hizi zikifuata vigezo vilivyowekwa nina uhakika hata madereva watakaozalishwa watakuwa bora," amesema SACP Ng'anzi.

Mnamo Februari 22, 2023, Mhe. Mha. Hamad Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitangaza kuwa madereva wote wa vyombo vya moto kibiashara wahakikishe wamesajiliwa LATRA kabla ya tarehe 30 Aprili, 2023, madereva mbalimbali wameweza kujitokeza ili kufanyiwa usajili ambapo mpaka sasa takribani madereva 3334 wamejitokeza na kufanyiwa usajili.




***Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi ya LATRA mkoa wa Dar es Salaam, kulia kwake ni Salum Pazzy Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano - LATRA***

# TABOA: HATUVUTANI NA LATRA

Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) kimekanusha madai ya kuwepo kwa mvutano baina yake na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kama ilivyoripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari nchini siku ya Jumatano Mei 3, 2023.

Hayo yamesemwa na Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), wakati wa mkutano na wanahabari ulioandaliwa na LATRA kwa kushirikiana na TABOA uliofanyika katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Jumatano Mei 3, 2023.

Akizungumza na wanahabari Bw. Joseph amesema hakuna viashiria vyovyote vya kutokuelewana na LATRA kwani wamekuwa wakishirikiana katika mambo mbalimbali, huku wakishirikishwa katika kila jambo la maamuzi linalowahusu.

“Kumekuwa na sintofahamu kuwa kuna mvutano baina yetu na LATRA jambo ambalo sio kweli, sisi na LATRA tunashirikiana kwa kiasi kikubwa tofauti na inavyosemekana, tumeshirikiana katika mambo mengi kama upangaji wa nauli za mabasi, suala la Tiketi Mtandao tumekuwa tukiitwa ili tutoe maoni, kimsingi uongozi wa LATRA umekuwa ukitufikia kwa wakati,” amesema Bw. Joseph.

Aidha, Bw. Joseph ameelezea hitaji la TABOA kwa taasisi za serikali kama vile Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Jeshi la Polisi kuendelea kuwawekea mazingira rafiki ili kuboresha sekta ya Usafiri nchini.

“Ombi langu kwa TAMISEMI na Jeshi la Polisi watuboreshee zaidi stendi zetu na hali ya usalama ili dira yetu ya kusafiri saa 24 iweze kufikiwa kwa haraka,” amesema Bw. Joseph.

Kwa upande wake Bw. Salum Pazzy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka LATRA, ameeleza kuwa ili kufanya kazi zake kwa ufanisi LATRA imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali ambao moja kwa moja wanahusika na sekta ya usafiri ardhini.

“Napenda kuwashukuru wadau mbalimbali ambao tumekuwa tukishirikiana nao tunapofanya kazi zetu za udhibiti, wakiwemo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na TABOA. Wadau kama TABOA ndio wanaotegemewa na Serikali ili kutoa huduma maana Serikali haina mabasi na wala haifanyi biashara, hivyo nawashukuru kwa kushirikiana katika mambo kama uanzishwaji wa Tiketi Mtandao,” amesema Bw. Pazzy.

Vilevile ameeleza kuwa Mamlaka ilianza majaribio ya safari za usiku kwa kuanza na safari za alfajiri mnamo Disemba 2022 ambapo kwanzia Mei mwaka huu Mamlaka imeanza kutoa ratiba kwa safari za mabasi kuanzia saa 9 usiku.

“Baada ya hoja zilizotolewa na waheshimiwa Wabunge, pamoja na kupokea maelekezo kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Mhe. Mha. Hamad Masauni (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama kikosi cha Usalama Barabarani na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Mamlaka ilifanya majaribio ya safari za usiku kwa kuanza na safari za alfajiri mnamo Disemba 2022, zaidi ya mabasi 180 sasa yamepatiwa ratiba ya kusafiri kwanzia alfajiri, na mpaka Mei 1, 2023 Mamlaka imeanza kutoa ratiba kwa mabasi yenye uhitaji wa kuanza safari kwanzia saa 9 usiku,” ameeleza Bw. Pazzy.

LATRA imekuwa ikifanya Mikutano na wadau mbalimbali ili kuweza kuboresha hali ya usafirishaji nchini, Mamlaka imekuwa ikiwaita wadau mbalimbali na kupokea maoni ili kuona namna bora ya kuboresha sekta ya usafiri, mikutano ya kujadili mambo kama nauli za mabasi, matumizi ya Tiketi Mtandao na nauli za daladala iliitishwa, wadau wakafika na kutoa maoni yao ambayo yalifanyiwa kazi.

# MADEREVA BAJAJI NA BODABODA WAASWA KUJIWEKEA AKIBA ILI KUJIKWAMUA KIUCHUMI

Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw, Johansen Kahatano amewasihi wamiliki na madereva wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda) na matatu (bajaji) mkoani Kilimanjaro kuanza tabia ya kujiwekea akiba ya fedha ili kuweza kujikimu kiuchumi.

Bw. Kahatano amesema hayo kwenye kikao cha kupokea taarifa ya Kamati ya Uratibu wa Mchakato wa Uanzishwaji wa Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa wamiliki na madereva wa pikipiki za magurudumu wawili (bodaboda) na matatu (bajaji) kilichofanyika Mei 4, 2023 katika ukumbi wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Manispaa ya Moshi mjini Mkoani Kilimanjaro.

Vilevile, Bw. Kahatano amesema, kazi ya kuendesha bajaji na bodaboda ni kama kazi nyingine, hivyo amewakumbusha madereva na wamiliki hao kuheshimu na kuonesha weledi wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao,"Nawasihi kuwa mabalozi wazuri kwa madereva wenzenu kote nchini kwa kufuata Sheria na Taratibu za Usalama Barabarani ili kuepuka ajali ambazo zinapunguza nguvu kazi ya Taifa."

Naye Bw. Patrick Boisafi, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua mchango wa maafisa wasafirishaji nchini na imeweka ahadi ya kuwasaidia vijana kupitia vyama vya ushirika.

"Nawapongeza sana LATRA, Jeshi la Polisi na kamati nzima kwa kutekeleza maono ya Serikali yetu na niwasihi sana walengwa kuwa muendelee kuwa na umoja na mshikamano ili kufikia malengo mliyojiwekea. Mtafundishwa jinsi ya kuweka akiba, mkazingatie na muwe na utaratibu wa kuweka akiba kidogokidogo," amesisitiza Bw. Boisafi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Bw. Mohammed Nkya ambaye pia ni mjumbe wa Kamati ya Uratibu wa Mchakato wa Uanzishwaji SACCOS hiyo amesema wataendelea kushirikiana na wamiliki na madereva wa bajaji na bodaboda Mkoani hapo na kuhakikisha wanajikwamua kiuchumi.

Akizungumzia faida za SACCOS kwa madereva na wamiliki wa bodaboda na bajaji, Afisa Mfawidhi wa LATRA mkoa wa Kilimanjaro Bw. Paul Nyello amesema itawasaidia katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi, itakuwa rahisi kwa Mamlaka kuwaratibu wakiwa katika majukumu yao, itawasaidia kukua kiuchumi na kuweza kusaidiana wao wenyewe na kikubwa zaidi itaongeza heshima ya kazi wanayoifanya.



*Bw, Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara (LATRA) pamoja na maafisa wengine wakiwapokea maafisa usafirishaji waliohudhuria katika ufunguzi wa Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) Manispaa ya Moshi Mjini, Kilimanjaro.*



***Mhe. Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, akizungumza na Maafisa Usafirishaji katika semina ya mafunzo iliyofanyika katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.***

# MHE BABU: ZINGATIENI SHERIA, MIONGOZO NA TARATIBU ZA USAFIRISHAJI

Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Mhe. Nurdin Babu amewaasa madereva wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda) na matatu (bajaji) kuzingatia Sheria, Miongozo na Taratibu za usafirishaji pindi wanapokuwa katika majukumu yao.

Mhe. Babu amesema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuanzisha chama cha ushirika cha watoa huduma za usafirishaji kwa njia ya bajaji na boda boda katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Mjini na Moshi Vijijini tarehe 05 Mei, 2023 katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa, Kilimanjaro.

"Kwa sasa tuna watoa huduma wengi wa usafirishaji kwa njia ya bajaji na boda boda katika Mkoa wetu. Wingi wetu unatakiwa kuendana sambamba na kuzingatia Sheria, Taratibu na kuhakikisha kuwa huduma tunazotoa zinakuwa za uhakika, kistaarabu, kuheshimiana na kushirikiana," ameeleza Mhe. Babu.

Vilevile amewapongeza kwa kukubali na kushiriki katika kuanzisha ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) utakaowawezesha kupata fursa ya kujiwekea taratibu za utoaji huduma za usafirishaji, kupata mitaji kwa ajili kuboresha au kuongeza huduma pamoja na kupata elimu ya mara kwa mara ya biashara, usalama barabarani na masuala mengine na kukopeshana vitendea kazi.

Naye Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw. Johansen Kahatano amesema SACCOS hiyo itawasaidia kuboresha maisha yao kijamii na kiuchumi kwa kuwa wataweza kukopesheka kupitia hisa zao na hatimaye kutoka kwenye kuajiriwa na kuwa na uwezo wa kujiajiri.

"LATRA tupo pamoja na nyie katika hili na kupitia ushirika huu mtapata kamisheni ambayo itawasaidia kujikwamua kiuchumi na hivyo mtaweza kujitegemea. Kikubwa mjiepushe na migogoro isiyo na tija ili kufikia dira na malengo mliyojiwekea," amesisitiza Bw. Kahatano.

Vilevile amewataka madereva hao kuwa mabalozi katika kuhamasisha na kuratibu tuoaji wa elimu kwa watoa huduma wengine katika vituo mbalimbali vilivyopo Mkoani humo.

Kwa nyakati tofauti, madereva wa bajaji na bodaboda Mkoani Kilimanjaro wameishukuru LATRA, Jeshi la Polisi pamoja na Kamati ya Uratibu wa Mchakato wa Uanzishwaji wa Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa kuwezesha ushirika huo kwa kuwa utawasaidia katika kuanzisha miradi ya maendeleo itakayobadili maisha yao kiuchumi.

# SILANDA: TUMIENI SACCOS KUJIKWAMUA KIJAMII NA KIUCHUMI




***Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira kutoka LATRA Bw. akizungumza na Maafisa Usafirishaji mkoani Kilimanjaro.***

Meneja Uratibu Usalama na Mazingira kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw. Geoffrey Silanda amewaasa wamiliki na madereva wa pikipiki za magurudumu Mawili (Bodaboda) na Matatu (Bajaji) kutumia vizuri Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ili kujikwamua kijamii na kiuchumi.

Bw. Silanda amesema hayo wakati akifunga mafunzo ya Ushirika kwa wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa wamiliki na madereva wa pikipiki za magurudumu mawili (boda boda) na pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi Mjini na Moshi Vijijini uliofanyika Mei 16, 2023 katika ukumbi wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Manispaa ya Moshi mjini Mkoani Kilimanjaro.

"kwa kupitia ushirika huu, mtapata manufaa mengi ikiwa ni pamoja na fursa ya kujiwekea taratibu za utoaji huduma za usafirishaji, kupata mitaji kwa ajili kuboresha au kuongeza huduma, kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo, kujikwamua kutoka kwenye kuajiriwa mpaka kujiajiri kwa kuweza kununua bajaji na bodaboda zenu wenyewe pamoja na kupata elimu ya mara kwa mara ya biashara, usalama barabarani na masuala mengine ikiwemo kukopeshana vitendea kazi," amesema Bw. Silanda.

Vilevile amesema kuwa, Mamlaka inafanya jitihada kubwa ya kuboresha sekta ya usafiri wa bodaboda na bajaji na moja ya jitihada ni kusaidia uanzishwaji wa vyama vya ushirika kwa wamiliki na madereva wa vyombo hivyo, "Niwahakikishie kuwa Mamlaka ipo pamoja na ninyi wanaushirika katika kuhakikisha chama kinaleta manufaa chanya kwenu ninyi. Katika hili tumekuwa pamoja kuanzia upokeaji wa taarifa ya kamati ya uratibu kuhusu uanzishwaji wa ushirika huu, tukazindua mafunzo kwa pamoja na leo tunahitimisha mafunzo yetu kwa pamoja."

Naye Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoani Kilimanjaro SSP. Pili Misungwi amewakumbusha madereva bodaboda na bajaji kuzingatia Sheria za Usalama barabarani ili kuwa na usafiri salama na wenye tija nchini.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa wamiliki wa bodaboda na bajaji Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Hamad Bendera ameishukuru LATRA kwa kuratibu uanzishwaji na mafunzo ya SACCOS hiyo na wameahidi kuwa mfano bora kwa kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Bw. Mohammed Nkya ambaye pia ni mjumbe wa Kamati ya Uratibu wa Mchakato wa Uanzishwaji SACCOS hiyo amesema wataendelea kushirikiana na wamiliki na madereva wa bajaji na bodaboda Mkoani hapo na kuhakikisha wanafanikisha azma ya uanzishwaji wa SACCOS hiyo.



***Baadhi ya wafanyakazi wa LATRA na wajumbe wa Jopo la kufuatilia maamuzi ya LATRA wakifuatilia wasilisho la majukumu ya LATRA kwa mujibu wa Sheria.***

# JOPO LA KUPITIA MAAMUZI YA LATRA LAZINDULIWA

Jopo la kupitia maamuzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) linaloundwa na wajumbe wa nne (4) limezinduliwa rasmi Juni 2, 2023 katika ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Jopo hilo, Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amesema kuwa, Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA kupitia kikao chake maalum kilichofanyika Dodoma tarehe 7 Februari, 2023, iliwateua wajumbe wa nne (4) wa Jopo hilo ambao ni Bw. Mohamed R. A. Mpinga, Mhandisi John Ngaraguza, Wakili Theresia Michael Clemence, pamoja na Wakili Asma Selemani Mohamed.

Aidha, CPA Suluo amesema, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA Prof. Ahmed Mohamed Ame, alimteua Bw. Mohamed R. A. Mpinga kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Mapitio. Bw. Mpinga ni Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mstaafu.

Vilevile amesema, Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA kwa mujibu wa kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 inapaswa kuunda Jopo la kupitia maamuzi ya Mamlaka linalohusisha watu wawili (2) wenye uzoefu wa masuala ya Sheria na waliofanya kazi kwa angalau miaka kumi (10) pamoja na watu wawili (2) wenye uzoefu wa angalau miaka kumi (10) kwenye masuala ya Uchumi, Fedha, Uhandisi au Usimamizi wa Usafiri.

CPA Suluo ameongeza kuwa, maamuzi yatakayoshughulikiwa na jopo hilo ni kwa mujibu wa kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kwa mtu yeyote ambaye hatoridhishwa na maamuzi ya Mamlaka anaweza ndani ya siku 14 tangu kutolewa maamuzi hayo, kuomba maamuzi hayo yapitiwe,

CPA Suluo amesema, "Tunaishukuru Bodi yetu kwa kuwateua na tunaamini mtatekeleza majukumu yenu kwa weledi wa hali ya juu kwa kuzingatia kuwa Mamlaka inatoa maamuzi na endapo mtoa huduma hajaridhishwa na maamuzi hayo basi atawasilisha kwenu ili kupitia upya maamuzi tuliyoyafanya na hatimaye jopo litatoa mapendekezo yake kwa Bodi ili iweze kufanya maamuzi kwa jambo husika. Endapo maamuzi hayo hayataridhiwa na mleta maombi, anaweza kukata rufaa kwa Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal-FCT) kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413," ameeleza CPA Suluo.

Baada ya uzinduzi huo, wajumbe hao wamepewa semina ya Sheria, Kanuni, wajibu na majukumu ya Mamlaka ili ziwaongezee uelewa wakati wa kutekeleza majukumu yao.

# LATRA: ZINGATIENI SHERIA ZA USALAMA BARABARANI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewasihi watumiaji wa huduma za usafiri ardhini kufuata Sheria, kanuni na Taratibu za Usalama Barabarani ili kuepuka ajali na madhila mengine yanayoweza kutokea.

Hayo yamesemwa na Bw. Salum Pazzy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kutoka LATRA wakati wafanyakazi wa LATRA walipotembelea Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) na kushiriki zoezi la Uchangiaji Damu ikiwa ni sehemu ya kurudisha kwa jamii katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Juni 21, 2023.

Akizungumza baada ya kuchangia damu Bw. Pazzy amesema, baadhi ya watumiaji wa huduma za usafiri ardhini wamekuwa na tabia ya kupuuzia Sheria za Usalama Barabarani na wengine kushabikia uvunjifu wa Sheria hizo, hali inayowaweka katika hatari ya kupata ajali na madhila mengine barabarani.

"Ningependa kuwasihi wasafirishaji na watumiaji wengine wa huduma za usafiri ardhini kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Usalama Barabarani, kwani kwa kufanya hivyo wanaweza kujiepusha na changamoto mbalimbali wawapo safarini kama ambavyo tumeshuhudia wenzetu ambao wapo hapa hospitali kwa sababu ya ajali, hivyo ni vyema kujiepusha na tabia hatarishi pamoja na kushabikia tabia hizo," amesema Bw. Pazzy.

Akizungumzia sababu za LATRA kwenda katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) Bw. Jonathan Kitururu, Mratibu wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu kutoka LATRA amesema wahanga wengi wa ajali za barabarani wanatibiwa MOI hivyo imekuwa rahisi kuwafikia na kuwapa faraja.

"Asilimia kubwa ya waathirika wa ajali za barabarani ni bodaboda na bajaji, hivyo watu hawa ni wahitaji haswa wa damu na wanatuhusu moja kwa moja, hivyo tukaona ni vyema kuja hapa (MOI) na kushiriki zoezi la kuchangia damu," amesema Bw. Kitururu.

Naye Bw. Patrick Mvungi, Meneja Uhusiano kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) amewashukuru wafanyakazi wa LATRA kwa kufika na kushiriki zoezi la kuchangia damu huku akiwaasa wananchi wengine kujitokeza na kuchangia damu kwani kwa kufanya hivyo wanasaidia kuokoa maisha.

"Tunawashukuru sana ndugu zetu wa LATRA waliotenga muda wao kufika hapa (MOI) na kushiriki zoezi la kuchangia damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wetu. Hapa MOI mahitaji ya damu ni makubwa sana wastani wa chupa 15 hadi 30 kwa siku, ukizingatia kwamba tunapokea idadi kubwa ya majeruhi wanaohitaji kufanyiwa upasuaji na kuongezewa damu, hivyo nitoe wito kwa Taasisi nyingine na Watanzania kwa jumla kujitokeza na kuchangia damu kwani kwa kufanya hivyo tunaokoa maisha ya watu wengi," amesema Bw. Mvungi.

Akizungumza baada ya kuchangia damu Bi. Lilian Temu, Afisa Huduma kwa Wateja LATRA ameelezea hali aliyoipitia wakati akichangia damu, "Nimefurahi sana kuchangia damu naamini itaokoa maisha ya mtu, hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia damu, mwanzoni nilikuwa na hofu sana, niliwaza labda nitapata kizunguzungu au nitadondoka au hata kuugua, lakini baada ya kuchangia damu hofu yote imeondoka na ninajiona ni mzima kabisa, hivyo watu waache uoga na wajitokeze wachangie damu," amesema Bi. Lilian.

Asilimia kubwa ya ajali za barabarani zinasababishwa na makosa ya kibinadamu kama vile mwendokasi uliopitiliza na kupuuzia alama za barabarani, madhara ya ajali hizo husababisha kupoteza maisha au kupoteza viungo vya mwili na hivyo kupoteza nguvu kazi ya Taifa. Hivyo ni vyema kwa watumiaji wa huduma za usafiri ardhini kufuata Sheria za Usalama Barabarani na kuacha kushabikia uvunjaji wa Sheria hizo ili kufanya Usafiri Ardhini kuwa salama.



***Baadhi ya wafanyakazi wa LATRA waliojitokeza kwenye zoezi la kuchangia damu wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI).***

# MHE MALISA: ZINGATIENI SHERIA NA KANUNI ZA USAFIRISHAJI



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Mhe. Beno Malisa amewaasa wasafirishaji wa abiria na mizigo Mkoani Mbeya watimize wajibu wao kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za usafirishaji.

Mhe. Malisa amesema hayo Juni 26, 2023 kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homera katika mkutano wa wadau wa usafirishaji abiria na mizigo ulioitishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kujadili changamoto za usafirishaji.

"Kwa kuwa jukumu hili la kujadili na kutoa maoni ya uboreshaji huduma za usafirishaji lipo kisheria, basi nawasihi kila mmoja wetu kwa kuzingatia umuhimu wa kazi hii atimize wajibu wake kwa umahiri wa hali ya juu," ameeleza Mhe. Malisa

Pia, ameipongeza LATRA kwa kuandaa mkutano huo na kuwa hatua hiyo inaonesha LATRA inavyowajali watoa huduma wa usafiri ardhini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo amesema sekta ya usafirishaji ni moja kati ya sekta muhimu nchini kwani kila mmoja anahitaji huduma hii ya usafiri ili kutimiza wajibu wake wa kila siku.

"Huduma hii ya usafiri ni ya umuhimu katika jamii yoyote na ina mchango mkubwa katika uchumi na ustawi wa jamii yoyote ile duniani hata kufika hapa wote tumekuja kwa usafiri wa aina mbalimbali," ameeleza CPA Suluo.

Vile vile amewapogeza wadau wa usafirishaji wa abiria na mizigo mkoani humo kwa kuacha shughuli zao muhimu na kuhudhuria mkutano huo.

Naye Mwenyekiti wa Wasafirishaji mkoa wa Mbeya Bw. Elias Mwanginde amesema kuwa, wasafirishaji wa mkoa huo wameona nuru kupitia uongozi wa sasa wa LATRA, hivyo watashirikiana kwa ukaribu ili kutekeleza mambo waliyokubaliana katika mkutano huo.

"Tunaona LATRA sasa ina uongozi imara na kutakuwa na mabadiliko, tunashukuru kwa elimu na majibu mazuri tuliyopata kwa maswali tuliyowauliza. Kupitia mkutano huu tumejulishwa kuwa Kituo cha LATRA cha Kutahini Madereva kiko tayari, pia leo hii tumetangaziwa fursa na wenzetu wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kuwa wako tayari kuwapiga msasa madereva wetu ili kuwakumbusha mambo ya kuzingatia wakatapoenda kufanya mtihani wa kuthibitishwa," amesema Bw. Mwanginde

Kwa upande wake, Bw. Muntazir Kassamia, msafirishaji wa mizigo amesema kuwa, mkutano huo umejenga uhusiano mzuri baina ya wasafirishaji na Serikali kwa kuwa baadhi ya changamoto zimeweza kutatuliwa kwa wakati na zingine zinafanyiwa kazi.

"Leo tumefarijika sana kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA katika mkoa wetu wa Mbeya na tulikuwa na changamoto zetu ndogo ndogo na tunashukuru kwa uweledi na busara zake kuna mambo mengine ameyapatia ufumbuzi papo kwa papo, baada ya kupewa elimu na uamuzi alioufanya kwa kweli ametengeneza uhusiano mzuri sana baina ya LATRA na wasafirishaji mkoani hapa," amesisitiza Bw. Kassamia.

Naye Kaimu Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa wa Mbeya SP Hussein Gawile amesema, "Kikao cha leo kimeleta hamasa kubwa sana kwa wamiliki maana leo wamepata ufumbuzi wa changamoto zao na mengi ambayo yamezungumzwa ni yale yatakayoleta athari chanya kwenye tasnia hii ya usafirishaji nchini."

LATRA imekua na utaratibu wa kuandaa mikutano mbalimbali ya wadau wa usafirishaji nchini kwa lengo la kutoa elimu pamoja na kuimarisha uhusiano baina ya Mamlaka na wadau wa usafirishaji ili kuleta maendeleo katika sekta ya usafiri ardhini nchini.

# MHA. KISAKA: KUWENI HURU KUTOA MAONI YENU

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) imewataka wadau wa Usafiri Ardhini kuwa huru na kujitokeza kwa wingi na kutoa maoni katika Rasimu za Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2023 ambazo zinajadiliwa katika mikutano ya wadau wa Usafiri Ardhini inayoendeshwa na Wizara hiyo.

Hayo yamesemwa kwa nyakati tofauti na Mhandisi Aroni Kisaka, Mkurugenzi wa Huduma za Usafiri kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) na Bw, Andrew Magombana, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri kwa Njia ya Barabara kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) ambao walimuwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Bw. Gabriel Migire walipokuwa wakifungua Mikutano ya wadau wa Usafiri Ardhini iliyofanyika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Mha. Kisaka amewaambia wadau hao kuwa, wanapaswa kuwa huru na kutumia nafasi hiyo vizuri kwani mchango wao ndio utakaosaidia kupatikana Kanuni bora, huku akiwahimiza kutumia njia zote za kutoa maoni.

"Nawaomba muwe huru mnapotoa maoni yenu na tumieni muda wenu vizuri, na siku 14 ambazo tumewapatia tumieni vizuri kwa kupitia vizuri Rasimu hizi, ili hata pale ambapo utakuwa umesahau kutoa maoni kwa siku ya leo basi uweze kutuma maoni yako katika anwani mtakazopatiwa," amesema Mha. Kisaka.

> **"matumaini yangu ni kuwa kutakuwa na dira nzuri katika sekta ya usafirishaji, hii ni kama maoni ambayo wadau tumeyatoa yatachukuliwa na kufanyiwa kazi**

Kwa upande wake Bw. Magombana amesema kuwa wakati LATRA inaendelea kutekeleza majukumu yake ya udhibiti, imekuwa ikikumbana na changamoto mbalimbali kama vile kutokuwepo kwa Kanuni mahususi za kushughulikia usafirishaji wa bidhaa hatarishi kwa upande wa barabara kama ilivyo kwenye usafiri wa Majini na njia ya Reli, kuwepo na baadhi ya wadau ambao wanapaswa kudhibitiwa lakini hawadhibitiwi hivyo kuleta athari mbalimbali katika tasnia zinazodhibitiwa.

Kutokuwepo kwa Kanuni mahususi zitakazoonesha utaratibu wa huduma za kimtandao kama vile Tiketi Mtandao na Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyombo vya Usafirishaji, na kuendelea kuwepo na kutumika kwa Kanuni ya iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Nchi Kavu na Majini (SUMATRA).

*Inaendelea uk.34 >>*



***Wadau mbalimbali waliojitokeza katika mikutano ya kujadili Rasimu za Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2023***



***Wadau mbalimbali waliojitokeza katika mikutano ya kujadili Rasimu za Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2023***

<< Inatoka uk.33

"Kwa kuzingatia hayo, Wizara kwa kushirikiana na LATRA tukaandaa rasimu hizi 8 ili kupata suluhu ya changamoto hizo. Tumeitisha vikao vya wadau ili kupata maoni yenu kwa kuwa ninyi ndio wadau wakuu katika hili na Kanuni hizi ni zenu," amesisitiza Magombana.

Kwa upande wake CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA amesema LATRA inafanya majukumu yake kwa mujibu wa Sheria kupitia Kanuni mbalimbali huku akiahidi ushirikiano baina ya LATRA na wadau wote wa Usafiri Ardhini.

"LATRA tunafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya LATRA Sura ya 413 pamoja na Sheria nyingine za Kisekta kama Sheria ya Reli ya mwaka 2017, kupitia Kanuni mbalimbali tunaweza kusimamia Sheria hizi ili huduma zitolewe kwa ufanisi zaidi, LATRA tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa uweledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zote zilizopo," amesema CPA Suluo.

Kwa upande wake Bw. Raymond Samson, mjumbe wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) amewasihi wadau wengine kujitokeza kwa wingi ili kutimiza haki yao ya Kikatiba.

"Kutokana na Mkutano huu, matumaini yangu ni kuwa kutakuwa na dira nzuri katika sekta ya usafirishaji, hii ni kama maoni ambayo wadau tumeyatoa yatachukuliwa na kufanyiwa kazi, hivyo niwasihi wadau wenginge kwenye kanda zingine ambazo mikutano hii itafanyika wajitokeze ili watimize haki yao ya Kikatiba," amesema Bw. Samson.

Naye Afisa Sheria Mwandamizi kutoka LATRA Bi. Mwadawa Sultan amezitaja Rasimu za Kanuni hizo nane (8) kuwa ni; Kanuni za Mamlaka Udhibiti Usafiri Ardhini za Uwezeshaji wa Huduma za Usafiri za Mwaka 2023 zinazolenga kuwadhibiti watoa huduma, bidhaa au vifaa vinavyowawezesha Watoa Huduma zinazodhibitiwa kufanya shughuli zinazodhibitiwa. Mfano Mawakala na wasambazaji wa vifaa vya ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo vinavyodhibitiwa, Kanuni za Mamlaka Udhibiti Usafiri Ardhini za Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vinavyotoa Huduma za Usafirishaji Kibiashara za Mwaka 2023; zinazolenga kutekeleza kifungu cha 5(1)(f) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413.

Vilevile amesema Kanuni nyingine ni; Kanuni za Mamlaka Udhibiti Usafiri Ardhini za Ufifilishaji wa Makosa za Mwaka 2023 zinazolenga kufuata utaratibu uliowekwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali kupitia Sheria ya Taifa ya Mashtaka Sura ya 430 katika kufifilisha makosa, Kanuni

Inaendelea uk.35 >>





***Wadau mbalimbali waliojitokeza katika mikutano ya kujadili Rasimu za Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2023***

<< Inatoka uk.34

za Leseni za Usafirishaji za Vyombo Vinavyosafirisha Bidhaa Hatarishi za Mwaka 2023 ambapo kumeonekana haja ya kuwa na Kanuni mahususi za Usafirishaji wa Bidhaa Hatarishi kama ilivyo kwa upande wa usafiri wa majini na reli. Vilevile ni suala la kimataifa katika kulinda afya na mazingira dhidi ya athari za bidhaa hatarishi zinazo safirishwa ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

Bi Mwadawa amezitaja Kanuni nyingine ambazo ni; Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma zinazodhibitiwa za Mwaka 2023; ambazo zimerithiwa kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) hivyo lengo la sasa ni kuzihuisha ziwe rasmi chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Kanuni za Mamlaka za Udhibiti Usafiri Ardhini za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mwaka 2023 ambazo zimerithiwa kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) hivyo lengo la sasa ni kuzihuisha ziwe rasmi chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

"Kanuni nyingine tunazokusanya maoni ya wadau ni Kanuni za Mamlaka za Udhibiti Usafiri Ardhini za Matumizi ya Tiketi Mtandao za Mwaka 2023 zinazolenga kuweka utaratibu wa kuwatambua kwa kuwasajili na kuweka masharti juu ya kuendesha mfumo wa Tiketi Mtandao bila kupelekea usumbufu wa Watoa Huduma pamoja na Kanuni za Mamlaka za Udhibiti Usafiri Ardhini za Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa vyombo vya Usafirishaji Kibiashara zinazolenga kudhibiti wasambazaji wa vifaa vinavyotuma taarifa kwenye Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Vyombo na kuweka vigezo na masharti ya kufanya usambazaji huo," ameeleza Bi. Mwadawa.

Mei 08, 2023 Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) alitoa Taarifa kwa Umma kuhusu Mikutano ya Kupokea Maoni ya Wadau Kuhusu Rasimu za Kanuni Mpya za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kwa tarehe 15, 17 na 19 inayofanyika Kanda ya Kati, Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa pamoja na Kanda ya Mashariki.

> **"siku 14 ambazo tumewapatia tumieni vizuri kwa kupitia vizuri Rasimu hizi, ili hata pale ambapo utakuwa umesahau kutoa maoni kwa siku ya leo basi uweze kutuma maoni yako katika anwani mtakazopatiwa**

# HABARI PICHA



*Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisalimiana na baadhi ya viongozi mbele ya banda la LATRA katika ufunguzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2023 jijini Mwanza.*





*Mhe. Adam Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akipatiwa elimu ya udhibiti alipotembelea banda la LATRA kwenye Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2023 jijini Mwanza.*



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA akifuatilia utekelezaji wa masharti ya leseni kwa wasafirishaji waliopo Stendi kuu ya mabasi Magufuli*



*Mhe. Atupele Mwakibete, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi - Uchukuzi (wa tatu kutoka kushoto), CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA (wa pili kutoka kushoto) pamoja na viongozi wengine kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakishiriki Bonanza la Uchukuzi lililofanyika katika viwanja vya UDSM.*



*Baadhi ya wafanyakazi wa LATRA waliojitokeza kwenye zoezi la kuchangia damu wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI).*





**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kikiongozwa na Bodi ya Wahariri**

**Mwenyekiti:** CPA HABIBU SULUO | **Mhariri Mkuu:** SAMUEL KEENJA | **Wahariri Wasaidizi:** SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE | **Waandishi:** MAMBWANA JUMBE, MARIAM NINA, DEUSDEDITY MASEMBA | **Msanifu Picha:** IBRAHIM SAID | **Wapiga Picha:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA | **Wasanifu Jarida:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA